AMBOLA

SEASON 05

PALE MASHUJAA WANAPOLISALITI TAIFA LAO

MTUNZI: PATRICK.CK



HADITHI HII NI MALI YA MWANDISHI NA HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA KWA HIYO HAIRUHUSIWI KUCHAPISHA, AU KUITUMIA KWA NAMNA NYINGINE HADITHI HII BILA RUHUSA YA MWANDISHI.HATUA KALI ITACHUKULIWA KWA YEYOTE ATAKAYEKIUKA MASHARTI HAYA..

HADITHI HII NI YA KUBUNI HAINA MAHUSIANO NA TUKIO LOLOTE LA KWELI.

SIMULIZI NYINGINE ZA MTUNZI PATRICK.CK

SIMULIZI ZA MAPENZI

1.MISS TANZANIA
2.SERENA
3.BEFORE I DIE
4.BEYOND PAIN

SIMULIZI ZA UPELELEZI

5.PENIELA
6.QUEEN MONICA
7.THE FOOTBALL
8.I DIED TO SAVE PRESIDENT
9.KIAPO CHA JASUSI
10.KIKOSI CHA SIRI
11.SIRI
12.SCANDAL(KASHFA)
13.CAPTURE OR KILL MISSION
14.JAMII YA SIRI

MAWASILIANO
0764294499

© 2020 Masimulizi.Haki zote zimehifadhiwa

ILIPOISHIA SEHEMU ILIYOPITA

“Hallow” alisema Ruby

“Ruby naomba kuzungumza na Mathew Mulumbi tafadhali” alisema Faraji.Ruby alimpa simu Mathew ili azugumze na Faraji.

“Hallow” alisema Mathew

“Mathew kuna taarifa yoyote mmeipata alfajiri hii? Aliuliza Faraji, Sauti yake ilionesha wasi wasi mkubwa.

“Tangu tumerejea kutoka msituni hakuna taarifa yoyote tumeipata.Kuna taarifa gani? aliuliza Mathew.Faraji alivuta pumzi ndefu.Alionekana kutafuta aanzie wapi.

“Faraji kuna nini? Aliuliza Mathew.

“Nimepokea taarifa mbaya kuhusu Gavana”

“Kafanya nini Gavana? Aliuliza Mathew.

“Ametekwa na watu wasiojulikana alfajiri ya leo wakati akielekea

kanisani.”alisema Faraji.Mathew alishituka na kuuliza.

“Ametekwaje ?

“Gavana ana kawaida ya kuhudhuria ibada kila siku alfajiri.Dakika chache baada ya kutoka nyumbani kwake zilitokea gari mbili na kulizuia gari lake.Walishuka watu wenye silaha na kuwapiga risasi dereva na walinzi watatu halafu wakamchukua Gavana.Mpaka sasa haijulikani mahali alipo. Jeshi la polisi wanaendelea kumtafuta.

Baada ya kupata taarifa hizo nimeona nikujulishe mara moja ili muwe makini.Hali ni mbaya” alisema Faraji.

“Ahsante sana Faraji kwa taarifa hii.Vipi kuhusu wewe unadhani utakuwa salama mahali ulipo? Aliuliza Mathew.

“Sifahamu Mathew lakini pale nitakapohisi hatari nitawajulisha mara moja” alisema Faraji na kuagana na Mathew.

“Kuna nini Mathew? Aliuliza Gosu Gosu.

“Gavana ametekwa nyara na watu wasiojulikana alfajiri ya leo.Hali inazidi kuwa mbaya” alisema Mathew.Kilipita kimya kifupi halafu akasema

“Ambola tayari kumepambazuka.Unatakiwa kurejea katika makazi yako.Unaweza ukatafutwa ukakosekana yakaibuka maswali mahali ulipo.” Alisema Mathew.Ruby aliichukua simu ya Ambola akaiwekea ile program maalum halafu akampatia

mkufu wenye kamera akamuelekeza namna ya kuutumia.Jackline Mo alipewa miwani myeusi yenye kamera.Wote walipewa vifaa vya kuweka sikioni kwa ajili ya mawasiliano kisha wakaondoka.

“Jamani, hamjalala usiku wa kuamkia leo lakini fahamuni hakutakuwa na hata dakika moja ya usingizi hadi pale tutakapohakikisha tumeiharibu mipango yote ya mabeberu na kuwafagia vibaraka wao.Kutekwa kwa

Gavana nina uhakika mkubwa kuna mahusiano na hiki kinachoendelea.Imeongezeka kazi nyingine ya kumtafuta na kuhakikisha anakuwa salama.Tuna mlima mrefu wa kupanda.” Alisema Mathew na kunyamaza baada ya simu ya Ruby kuita.

“Faraji anapiga tena” alisema Ruby na kumpatia Mathew simu akaipokea.

“Hallow” alisema Mathew.

“Mathew nimejulishwa kuna wa wamenifuata hapa nyumbani wanadai ni

wanausalama wanahitaji nionane nao.Unanishauri nini? Nina hofu sana.”Aliuliza Faraji.

“Run !” Alisema Mathew

“Tafuta namna ya kutoka hapo nyumbani kwako bila kuonana nao. Kama nyumba yako ina mlango wa dharura, toka haraka kisha tujulishe. Hao siyo wanausalama. Tayari wamefahamu ulionana na Gavana usiku wa kuamkia leo.” Alisema Mathew.

“Sawa Mathew nitakujulisha nikitoka hapa

ndani” alisema Faraji na kukata simu.

“Tayari kumeanza kuchafuka.Naamini kile kilichofanyika usiku wa kuamkia leo tayari wamekifahamu. Kwa sasa tujitahidi kumuokoa Faraji Dilele ambaye jamaa wanamuwinda naye wampate. Ni yeye aliyetuwezesha tukaweza kuingia na kutumia mfumo wa SNSA. Gosu Gosu najua umechoka lakini hakuna muda wa kupumzika. Twende

haraka kumsaidia Faraji”
Alisema Mathew.

ENDELEA.....

Gari aina ya Landcruiser V8 rangi nyeupe, liliwasili Giraffe royal hotel. Dereva wa gari lile alishuka haraka haraka akafungua mlango wa upande wa kushoto, akashuka Jaji mstaafu Perfect Lyimo. Milango ya kati kati ya gari lile nayo ilifunguliwa wakashuka watu watatu.

“Karibuni sana Tanzania.” Alisema jaji mstaafu Perfect ambaye hupenda aitwe mzee Perfect.

“Ahsante sana tunashukuru” alisema mmoja wa wageni kwa niaba ya wenzake.

“Hoteli nzuri sana hii. Nimependa muonekano wake usiku huu” alisema mwingine huku akitabasamu.

“Hii ni moja ya hoteli bora kabisa hapa Tanzania na Afrika Mashariki. Kwa hadhi yenu ninaamini hoteli hii

inawafaa sana” alisema Mzee Perfect huku akitabasamu.

Dereva alishusha mizigo ya wageni kutoka garini. Wahudumu walifika na toroli maalum wakaipakia mizigo ile.

Hawakuchukua muda mrefu mapokezi kwa sababu kila kitu tayari kilikwisha kamilishwa na wenyeji kabla wageni wale hawajafika nchini. Mizigo yao ilipelekwa katika mojawapo ya nyumba kadhaa zilizopo hotelini hapo. Ndani ya Giraffe Royal hotel, kuna nyumba zipatazo ishirini

ambazo ni maalum kwa wageni wajao kwa makundi au wale wajao na familia zao. Nyumba namba G 16 ndiyo walipewa wageni wale wa Perfect. Ilikuwa karibu kabisa na bahari.

“Wageni wetu poleni kwa safari ndefu na karibuni sana Tanzania.” Alianzisha maongezi mzee Perfect.

“Tunashukuru na tumefurahi sana kufika Tanzania. Mimi hii ni mara ya nne ninakuja Tanzania. Mara nyingine tatu nimekuja katika

safari za kitalii. Mara mbili na familia yangu, mara moja na marafiki zangu. Ninaipenda Tanzania ni nchi nzuri” alisema jamaa mmoja mwenye mwili mkubwa.

“Mimi ninaitwa Perfect Lyimo ni jaji mstaafu wa mahakama kuu lakini naomba mniite Perfect inatosha” alijitambulisha mzee Perfect.

“Mimi ninaitwa Azriel Blank” alijitambulisha yule jamaa mwenye mwili mkubwa ambaye alionekana kama ndiye kiongozi wa timu ile.

“Ninaitwa Efrayim Cowen” alijitambulisha mwingine ambaye alionekana kijana zaidi kuliko wenzake.

“Mimi ni Moshe Herson” alimalizia mgeni wa mwisho kujitambulisha. Huyu alikuwa amevaa fulana iliyokatwa mikono huku michoro ikionekana katika sehemu zilizokuwa wazi za mikono yake.

“Nimefurahi kuwafahamu. Kwa kuwa hivi sasa ni usiku mwingi nawaomba mpumzike halafu kesho tutakuwa na

mazungumzo muhimu ya kikazi. Mahali hapa ni salama kabisa msihofu chochote.” alisema mzee Perfect kisha akaagana na wageni wake akaelekea mahali liliko gari lake. Wakati akielekea maegesho ya magari, alichukua simu akaitafuta namba ya mke wake ili amfahamishe kuwa tayari wageni wamewasili. Alimpigia simu lakini haikupatikana.

“Bernadetha ana matatizo gani hadi amezima simu? Hii si kawaida yake” aliwaza Perfect. Alifunguliwa mlango

na dereva wake akaingia garini wakaondoka pale hotelibni. Perfect aliichukua tena simu akampigia mke wake lakini bado simu yake haikupatikana.

“Ninaamini huyu mwanamke atakuwa na mwanaume sehemu Fulani ndiyo maana amezima simu yake. Mimi na mke wangu tunaishi maisha ya ajabu sana. Ninachoshukuru ni kwamba watu hawafahamu kama mimi na mke wangu hatulali kitanda kimoja. Japo chumba ni kimoja lakini kila mtu ana kitanda chake. Mke wangu

yuko huru kufanya chochote akitakacho na mimi niko huru kufanya chochote nikitakacho. Hakuna anayemuonea wivu mwenzake au kumuuliza chochote kuhusiana na mambo anayoyafanya. Mapenzi kati yetu yalikwisha zamani sana kilichobaki ni ndoa tu ya makaratasi. Ninajilaumu sana kwa nini nilimuoa mwanamke yule. Sijawahi kuifurahia ndoa yangu hata siku moja tangu nimekuwa naye. Japo mbele za watu tunaonekana tunapendana lakini yote haya ni maigizo.Hakuna mapenzi

yoyote kati yetu. Mimi ni mtu mwenye hadhi kubwa lakini hakuna anayefahamu aina ya maisha ninayoishi. Mimi na mke wangu ni kama laana kwa mabo ya ajabu na aibu tunayoyafanya. Bernadetha amekuwa akitembea hadi na vijana wadogo kabisa. Mimi pia nimejikuta nikitembea hadi na Ambola mtoto ambaye tumempokea na kumlea kama mtoto wetu. Lakini sijutii nilichokifanya. Ambola amenirejeshea furaha japo sitaki afahamu aina ya maisha ambayo mimi na Bernadetha

tunaishi.” Aliwaza mzee Perfect na kutabasamu. Picha ya Ambola akiwa mtupu kitandani ilimjia kichwani akatoa tabasamu.

“Yule mtoto ni mzuri mno. Nimetembea na wanawake wengi lakini sijakutana na aliyeweza kunipa raha kama Ambola. Kuna wakati ninafikiria hata kumuoa kabisa awe mke wangu wa pili.” Aliendelea kuwaza Perfect na mara akakumbuka kitu.

“Nawaza siku ambayo Bernadetha atagundua

ninatembea na Ambola. Ataumia sana lakini potelea mbali kwani haya ndiyo maisha tuliyoamua kuishi. Nitamlinda Ambola kwa kila uwezo nilionao. Ninafikiria hata kuzaa naye mtoto ili kuimarisha zaidi mahusiano yetu" aliwaza Perfect akaichukua simu yake akampigia Margreth msaidizi wa Bernadetha.

"Mzee Pefect" alisema Margreth baada ya kupokea simu.

“Margrethj samahani kwa kukusumbua usiku huu”

“Bila samahani mzee Perfect. Unasemaje?

“Ninamuuliza Bernadetha. Uko naye?

“Hapana mzee Perfect siko naye. Niliachana naye muda mrefu kidogo akaniruhusu nirejee nyumbani kupumzika”

“Yeye alikwenda wapi?

“Hakuniambia anakwenda wapi mzee”

“Ahsante sana Margreth. Usiku mwema” alisema Perfect na kukata simu.

“Lazima atakuwa na mwanaume ndiyo maana amezima simu. Si kwamba ninamuonea wivu lakini ninamtafuta ili afahamu wageni tayari wamewasili” aliwaza Perfect.

Alifika nyumbani kwake na kitu cha kwanza alichokifanya ni kuingia bafuni akaoga kwa mara ya pili. Kisha oga alikaa kitandani.

“Niliwahi kusikia eti wapo wanawake ambao hutumia dawa Fulani kuwakamata wanaume. Wanadai dawa hiyo huwekwa katika mshumaa au koroboni na ikifika usiku taa zote huzimwa ukawashwa mshumaa au koroboi. Mwanamke akifanya hivyo mwanaume aliyemkusudia atateseka usiku kucha. Hatapata usingizi. Kila akifumba macho atamuona mwanamke huyo. Nyumba yake ataiona chungu. Atatamani hata usiku huo aondoke amfuate mwanamke.

Nahisi hivi ndivyo anavyonifanyia Ambola. Hapa nilipo naiona nyumba yangu kubwa kama kanisa. Natamani niondoke zangu hata sasa nirejee kwa Ambola.” Aliwaza Perfect akaishika simu akaitafuta namba ya Ambola akataka kumpigia akasita.

“Nitakuwa ninamsumbua yule mtoto. Mida hii pengine ameshalala. Ngoja niachane naye. Kutakapopambazuka kabla sijafanya chochote breki ya kwanza itakuwa kwa Ambola. Atanipitisha kwanza mzunguko mmoja ili mwili

ukae sawa” aliwaza mzee Perfect akajilaza kitandani.

“Akili yangu imehama kabisa. Kila sekunde ninamuwaza Ambola. Ninafikiria hata kumuondoa kabisa katika hizi operesheni zinazoendelea. Malaika kama yule hapaswi kabisa kushiriki katika misheni kama hizi za hatari. Kazi aliyofundishwa ni kutafuta taarifa muhimu kutoka kwa watu na hii inamfanya autumie mwili wake kama ulimbo wa kuwanasa wanaume ambao tunawalenga. Hili sitaki

liendelee. Ambola ni wangu peke yangu. Sitaki mwanaume mwingine amguse. Yule jamaa Gosu Gosu naye lazima auawe haraka sana. Inaonesha Ambola ameanza kumpenda. Alitaka kufahamu maendeleo yake. Kuna uwezekano mkubwa kama Gosu Gosu akiachiwa huru wanaweza wakasameheana na kurudiana. Sitaki hilo litokee. Nitahakikisha ndani ya kipindi kifupi kijacho anauawa.” aliwaza Perfect.

****

Mlio wa simu ya mkononi ulimtoa mzee Perfect usingizini. Alikuwa amelala usingizi usingizi mzito sana. Tangu alipojitupa kitandani aliporejea usiku hakugeuka hadi aliposhituliwa na mlio ule wa simu. Ilipata saa kumi na dakika mbili.

“Huu uchovu wote ni kazi ya Ambola jana usiku. Alinichezesha gwaride la uhakika” aliwaza huku akiinua mkono na kuichukua simu. Jina lilisomeka Dominic

Kengele. Perfect alishituka kidogo.

“Dominic kuna nini alfajiri hii.? Perfect aliuliza.

“Mzee samahani kwa kukusumbua, nakuomba ufike hapa hospitali kuu ya Mtodora haraka sana”

“Kuna nini huko hospitali?

“Kuna tukio limetokea. Ninaomba ufike hapa mara moja mzee” alisema Dominic.

“Dominic niweke wazi kuna nini hapo hospitali?

Tukio gani limetokea? Aliuliza Perfect.

“Mzee naomba usipoteze muda. Fika mara moja hapa hospitali” alisema Dominic na kukata simu.

Perfect alibaki katika mshangao mkubwa.

“Nni kimetokea? Alijiuliza na kuangaza angaza kila pembe ya chumba ndipo alipogundua mke wake hayupo.

“Bernadetha hajarerejea nyumbani hadi muda huu.

Amelala wapi? Alijiuliza akaitafuta namba ya mke wake akampigia lakini simu yake bado haikupatikana.

“Kwa nini simu ya Bernadetha haipatikani ? Hii si kawaida yake.” alijiuliza huku akiinuka na kuanza kujiandaa kwenda hospitali.

Dereva wake hakuwepo hivyo ilimlazimu kuendesha gari lake yeye mwenyewe. Bado kichwa chake kilijaa mawazo akijiuliza kile kilichotokea. Alipunguza mwendo wa gari akachukua

simu akampigia Margreth msaidizi wa mke wake.

“Mzee Perfect shikamoo” alisema Margreth baada ya kuipokea simu.

“Marahaba. Margreth umewasiliana na Bernadetha toka nilipokupigia usiku? Aliuliza Pefrect.

“Nilijaribu kumtafuta mara kadhaa lakini hapatikani simuni” alijibu Margreth.

“Ahsante Margreth” alisema Perfect na kukata simu.

“Yuko wapi Bernadetha? Pamoja na maisha haya tunayoishi lakini si kawaida yake kulala nje. Au kuna tatizo limempata ndiyo maana Dominic hataki kunijulisha? Alijiuliza Perfect.

Alifika hospitali akashuka haraka haraka na kumpigia simu Dominic akamjulisha kuwa tayari amefika. Dominic alimfuata akamchukua wakaenda kuketi sehemu.

“Dominic kuna nini? Aliuliza Perfect kwa wasi wasi.

“Mzee kuna jambo limetokea ambalo sikutaka kukueleza simuni”

“Nieleze tafadhali nini hasa kimetokea?

“Nilipigiwa simu na vijana walioingia zamu ya asubuhi katika safe house number 6. Nyumba hiyo ndimo alimokuwa amehifadhiwa yule jamaa Gosu Gosu. Kuna tukio baya limetokea katika nyumba hiyo.”

“Nini kimetokea Dominic? Tafadhali nieleze kila kitu, usizunguke!

“Mzee yamefanyika mauaji makubwa katika nyumba hiyo”

“Mauaji?

“Ndiyo mzee. Wameuawa walinzi wote waliokuwa wanalinda nyumba hiyo ambao jumla yao ni wanne. Vile vile imekutwa miili mingine ya watu wawili. Mmoja wa watu hao ni mama Bernadetha”

Mzee Perfect alihisi masikio yake yameziba ghafla. Kwa sekunde kadhaa hakuweza kusikia. Mara

alishituka kama mtu aliyetoka usingizini.

“Umesemaje Dominic? Aliuliza

“Pole sana mzee. Miongoni mwa watu waliouawa katika nyumba hiyo ni mama Bernadetha”

“Dominic tafadhali hili si jambo la kufanyia mzaha hata kidogo”

“Mzee ndiyo maana sikutaka kukwambia simuni. Tayari jeshi la polisi wamekwisha fika eneo la tukio

wameichukua miili hiyo na tayari imeletwa hapa hospitali kuhifadhiwa.”

Kilipita kimya kifupi. Picha mbali mbali zilikuwa zinapita katika kichwa cha mzee Perfect haraka haraka. Habari ile ya kifo cha mke wake ilimshitua sana.

“Mzee pole sana” alisema Dominic.

“Dominic , ah!.” Mzee Perfect alishindwa aseme nini.

“Mzee kama hutajali ninaweza kukupeleka

kukuonesha mwili wa mama Bernadetha” alisema Dominic.

‘Twende tafadhali”

Perfect aliinuka wakaelekea katika chumba cha kuhifadhi maiti. Perfect alihisi miguu mizito kila alivyozidi kupiga hatua kuelekea katika chumba cha kuhifadhia maiti.

“Bernadetha amekufa! Hii taarifa mbona inanipa mashaka kuiamini? Hadi nitakapoushuhudia mwili wake kwa macho yangu ndipo nitakapoamini kweli mke wangu amekufa” aliwaza

Perfect wakiwa wamekikaribia sana chumba cha kuhifadhia maiti. Dominic alizungumza na wahudumu wa chumba kile halafu akatoka akamfuata Perfect akamtaka waingie ndani. Perfect alipelekwa katika chumba ulimo mwili wa mke wake. Bado haukuwa umehifadhiwa katika jokofu. Perfect alihisi kama moyo wake unataka kuchomoka namna ulivyobadili mapigo yake baada ya kuuona mwili wa mke wake. Aliusogelea mwili ule taratibu akautazama vizuri ni kweli aliyelala juu ya

kitanda kile alikuwa mke wake Bernadetha. Alikuwa amepigwa risasi katika paji la uso. Perfect alifunika macho yake kwa viganja. Alishindwa kuyazuia machozi kumtoka.

“Oh Bernadetha mke wangu. Nani amekukatili uhai wako namna hii? Huu ni ukatili mkubwa sana” aliwaza Perfect akautazama tena mwili wa mke wake. Machozi yaliongezeka.

“Licha ya tofauti zetu, licha ya maisha ya laana tuliyoishi lakini bado nilikuwa

nakuhitaji sana katika maisha yangu. Bado kuna mambo ambayo siwezi kuyafanya bila wewe Bernadetha. Ni nani huyu aliyeitoa roho yako kikatili namna hii? Aliwaza Perfect.

Alinyoosha mkono akaushika uso wa mke wake.

“Bernadetha nitahakikisha ninamsaka mtu aliyekufanyia ukatili huu mkubwa. Nitahakikisha naye haendelei kuvuta pumzi. Naye lazima afe. Aliyenyoosha mkono wake akaingiza risasi katika kichwa

chako, mahali pekee salama kwake ni kaburini. Nitamsaka kila kona ya dunia hadi nihakikishe anapatikana. Umeondoka Bernadetha katika wakati ambao mipango yetu ambayo umeshiriki kuiandaa kwa muda mrefu imekaribia kukamilika. Ninakuahidi kila kitu lazima kitakamilika.” Aliwaza Perfect huku machozi mengi yakimbubujika.

Pole sana mzee” alisema Dominic akamshika mkono mzee Perfect akamtoa nje.

“Dominic nataka uniambie nani kafanya mauaji haya? Aliuliza Perfect.

“Mzee, mpaka sasa bado haijafahamika nani kafanya maujai haya. Ila tunadhani ni Gosu Gosu kwani ametoweka na hajulikani alipo”

“Ametoweka Gosu Gosu? Perfect alishituka.

“Ndiyo ametoweka. Tunahisi ni yeye aliyefanya mauaji hayo kisha akatoweka.”

Perfect aliwaza kwa muda halafu akachukua simu yake

akaitafuta namba Fulani iliyohifadhiwa kwa jina la Julius Mukoke akampigia.

“Mzee Perfect shikamoo” alisema Julius

“Sikiliza Julius. Kuna jambo kubwa limetokea usiku wa leo tunahitaji kukutana haraka sana.”

“Jambo gani?

“Bernadetha ameuawa.”

“Bernadetha? Julius alishangaa.

“Ndiyo. Si yeye peke yake bali kuna wengine watano

wakiwamo walinzi wanne waliokuwa wanalinda safe huse 6. Mtu aliyekuwa anashikiliwa katika nyumba hiyo Gosu Gosu ametoweka na hajulikani alipo inahisiwa ni yeye aliyefanya mauaji hayo”

“Perfect…”

“Julius tutazungumza mengi tukikutana. Nataka utume taarifa haraka katika mtandao wetu ili kila mmoja afahamu kilichotokea. Mimi niko hapa hospitali nitaondoka muda si mrefu kuanza taratibu za msiba lakini kabla sijafanya

chochote nataka viongozi tukutane kwa dharura tujadili hiki kilichotokea” alisema Perfect na kukata simu.

“Dominic, kumeanza kupambazuka na asubuhi hii taarifa za kifo cha mke wangu zitaanza kusambaa haraka sana. Maandalizi ya msiba yanatakiwa yaanze haraka. Kabla ya kueleka nyumbani nataka kuhudhuria kikao cha dharura. Naomba unipeleke ngome tafadhali” alisema Perfect. Dominic alimfungulia mlango Perfect akaingia garini kisha safari ikaanza kuelekea

Ngome mahali ambako mipango yao yote hufanyikia.

****

Ni kawaida ya Gavana wa benki kuu ya Tanzania, Jackson Mzumile kuamka kila siku usiku kuanzia saa tisa na kuingia katika chumba cha ibada kusali hadi inapotimu saa kumi na moja kamili ambapo hujiandaa kwa ajili ya kuhudhuria ibada ya misa katika kanisa lililo kilometa moja kutoka nyumbani kwake. Wakati Gavana akiwa katika maombi, ujumbe uliingia

katika simu ya mke wake. Hakuwa amelala, alinyoosha mkono akaichukua simu akaufungua ujumbe ule.

“Mauaji yamefanyika Safe house 6. Wameuawa watu 6 akiwemo mama Bernadetha. Gosu Gosu ametoweka. Anafahamu mengi ni mtu hatari sana kwetu. Tahadhari zichukuliwe kuanzia sasa. Mtajulishwa kile kinachoendelea. Julius”

Lucy mke wa Gavana aliurudia kusoma ule ujumbe akashusha pumzi. Haraka

haraka alitoka chumbani akaenda kuchungulia katika chumba cha ibada aliko mumewe, bado alikuwa anaendelea na maombi.

“Anakaribia kumaliza sala zake.” aliwaza na kurejea chumbani na kwa kasi akaichukua simu yake akafungua sehemu ya kuhifadhia majina akalitafuta jina Julius Mukoke akapiga.

“Madam Lucy” alisema Julius.

“Sikiliza Julius. Nimeupata ujumbe uliousambaza.

Nimeshituka sana. Mmewafahamu waliofanya tukio hilo? Aliuliza Lucy.

“Hapana bado hawajafaamika”

“Nadhani tunaweza kufahamu nani wamefanya tukio hilo.”

“Kivipi Madam Lucy?

“Mathew Mulumbi was here” alisema Lucy.

“Mathew Mulumbi? Julius alishangaa.

“Ndiyo. Alikuja hapa mara tatu jana. Mara ya kwanza

alikuja akazungumza na Gavana. Alimpa taarifa za mtu wake aliyeuawa Arusha. Baadaye alirejea tena. Kuna mtu mwingine alijiuinga nao katika mazungumzo.Ni Faraji Dilele”

“Faraji naye alijiunga katika mazungumzo pamoja na Mathew Mulumbi?

“Ndiyo. Yeye alipigiwa simu na Gavana kwa kutumia simu yangu akaja mara moja. Baada ya mazungumzo, Faraji aliondoka na Mathew Mulumbi sifahamu walielekea

wapi lakini baadaye walirudi tena. Faraji alichuka gari lake akaondoka. Nadhani walitoka katika kutekeleza mauaji hayo ili kumkomboa Gosu Gosu.”

“Hii ni taarifa iliyonishitua sana. Kama Faraji naye alifika hapo kuonana na Mathew Mulumbi ni wazi wao ndio waliofanya tukio lile.” Alisema Julius.

“Julius hawa watu si wa kufanyia mzaha hata kidogo. Kama Gavana ameanza kushirikiana na Mathew Mulumbi basi kila kitu

kitajulikana. Hatutakiwi kufika hatua hiyo. Mathew Mulumbi anatakiwa apatikane harka sana. Kuna watu wawili pekee hivi sasa wanaofahamu mahali alipo Mathew Mulumbi ambao ni Gavana na Faraji Dilele. Mkifanikiwa kuwapata hawa wawili Mathew atapatikana. Kwa sasa Gavana anamalizia maombi yake ya usiku na baada ya hapo atakwenda kanisani. Ni kawaida yake kuhudhuria ibada kanisani kila siku alfajiri. Nadhani muda huo ni muda mzuri kumchukua na kwenda

kumfanyia mahojiano. Nina uhakika ataeleza kila kitu.”

“Hilo ni wazo zuri sana Lucy. Ninawaandaa vijana wangu ili wafike eneo hilo ndani ya dakika chache zijazo. Unadhani amebakiza dakika ngapi atoke kuelekea kanisani?

“Ni zaidi ya nusu saa”

“Sawa. Timu ninayoituma watafika eneo hilo muda mfupi kuanzia sasa. Mara tu atakapotoka utanijulisha”

“Sawa nitafanya hivyo. Julius mkifanikiwa kumpata,

please don’t hurt him. Anatakiwa aulizwe maswali tu na ajibu. Sitaki aumizwe”

“Tutalizingatia hilo” alijibu Julius na kukata simu.

“Lazima ni Faraji ambaye ameendelea kumshawishi Jackson kufanya uchunguzi wa kupotea kwa Kelvin. Ninamchukia mno yule baba. Ni kwa sababu yake ndiyo maana Joseph hakati tamaa kutafuta wapelelezi. Kila mpelelezi mmoja anapouawa, anatafuta mwingine.” Aliwaza

Lucy halafu akajilaza kitandani.

Zilipita dakika tano tangu Lucy awasiliane na Julius, mlango ulifunguliwa akaingia Gavana akitokea katika chumba chake cha maombi. Aliingia bafuni kuoga halafu akajiandaa kwa ajili ya kuelekea kanisani kuhudhuria ibada ya kila siku asubuhi. Kabla hajatoka, alimfuata mke wake ambaye alijifanya amepitiwa na usingizi, akambusu halafu akatoka nje ambako aliwakuta dereva wake

na mlinzi tayari wamejiandaa. Aliingia garini akaondoka.

“He’s on move” Lucy alimtumia Julius ujumbe mfupi.

Garini, Gavana hakuwa na wasi wai wowote kama kuna tukio linakwenda kutokea dakika chache zijazo. Ghafla zilitokea gari mili zikienda kwa kasi kubwa. Dereva wa gari la Gavana alipunguza mwendo na kulisogeza gari pembeni ili kuzipisha gari zile. Gari moja ililipita gari la Gavana na kusima kati kati ya barabara

hivyo kumlazimisha dereva wa gari la Gavana kusimamisha gari. Kitendo kile kilimfanya mlinzi wa Gavana ahisi hatari. Alipogeuka nyuma aliliona gari lingine likiwa nyuma yao limesimama kati kati ya barabara. Aliitoa bastola yake lakini kabla hajachukua maamuzi yoyote risasi ilipenya katika kioo cha mbele na kuzama katika kichwa cha yule mlinzi. Sekunde mbili, dereva alitoa mguno baada ya kutandikwa risasi ya kichwa. Wavamizi wale hawakuhitaji kutumia nguvu tena kwani

tayari walifahamu ndani ya gari alibaki Gavana peke yake. Kioo cha dirisha kilipigwa mlango ukafunguliwa. Gavana alishushwa haraka haraka akavishwa mfuko kichwani akaingizwa katika gari lingine. Gari la Gavana lilikaguliwa simu yake ikachukuliwa kisha magari yale mawili yaliondoka kwa kasi kubwa.

****

Ndani ya kipindi kifupi baada ya kupata taarifa kutoka kwa Julius Mukoke, tayari watu kumi na moja walikutana mahali panapoitwa Ngome. Ni jumba kubwa la duara lililojengwa kati kati ya miti mingi. Ni katika nyumba hiyo ndimo Perfect na mtandao wake wamekuwa wakikutana kupanga mipango yao mbali mbali. Mtu wa mwisho kuwasili katika chumba kile alikuwa ni Julius Mukoke mkurugenzi wa SNSA. Baada ya kuwasili kikao kilianza kwa mwenyekiti kukifungua kikao.

“Ndugu zangu habari za asubuhi. Ninaanza kwa kuwashukuru nyote kwa kufika kwa haraka mara baada ya kupokea mwito. Pamoja na taarifa ya kukutana hapa kwa dharura ambayo wote tumeipata, lakini kuna tarifa nyingine ambayo naamini nyote mmeipata pia ya kifo cha mwenzetu, mpiganaji wetu madam Bernadetha. Nimeipokea taarifa hiyo kwa mshituko mkubwa kwani ni jana tulikuwa naye katika kikao cha mtandaoni akitupa taarifa ya mambo

yanavyokwenda. Sifahamu nani aliyefanya mauaji haya ambayo yana malengo ya kurudisha nyuma mipango yetu yote. Kabla hatujapokea taarifa yoyote, kwa niaba ya wezangu nataka nikupe pole sana jaji Perfect kwa msiba huu mkubwa. Naomba ufahamu kuwa msiba huu ni wetu sote kwa sababu Bernadetha alikuwa ndiye msimamizi mkuu wa shughuli zetu. Naweza kumuita mwanamke wa shoka kwa namna alivyokuwa anapambana kuhakikisha

misheni yetu inakwenda vyema. Nikisema nimuelezee Bernadetha nitachukua siku nzima, lkwani mambo aliyoyafanya ni mengi. Ni mtu aliyejitoa kwa hali na mali kuhakikisha misheni yetu inakamilika. Pole sana Perfect” alisema Charles Ombe mwenyekiti wa kikao kile.

“Ahsanteni sana ninawashukuru.” Alisema Perfect kukohoa kidogo kurekebisha koo.

“Kilichotokea hata mimi bado naona kama ni ndoto.

Bernadetha alinipigia simu akaniambia nikawapokee wageni wetu uwanja wa ndege, nikaenda. Nilipowafikisha wageni hotelini nilitaka kumjulisha kuwa wageni tayari wamefika lakini simu yake haikupatikana tena. Niliwauliza watu kadhaa na hata msaidizi wake akaniambia kuwa Bernadetha alimtaka akapumzike yeye kuna sehemu anakwenda. Alfajiri nilipigiwa simu na Dominic akanitaka nifike kwa haraka hospitali kuu ya Mtodora. Nilifika pale haraka

ndipo akanieleza kilichotokea. Sikuamini, nilitaka kuthibitosha kama nilichoelezwa ni kitu cha kweli. Niliingia ndani ya chumba cha kuhifadhi maiti nikaukuta mwili wa mke wangu. Ni kweli Bernadetha hatunaye tena. Ameuawa kikatili kwa kupigwa risasi kati kati ya paji lake la uso.” Perfect alishindwa kuendelea.

“Pole sana Perfect kwa kilichotokea. Dominic wewe ndiye msimamizi mkuu wa nyumba zetu zote za siri.

Tueleze nini hasa kilichotokea? Aliuliza Charles.

“Nilipigiwa simu na vijana wangu ambao waliingia katika zamu ya alfajiri kwamba kuna mauaji yametokea Safe house 6. Nilifika haraka eneo la tukio na kuthibitisha kilichotokea.Waliouawa ni walinzi wanne waliokuwa wanalinda nyumba hiyo, mama Bernadetha na mwingine ambaye alikutwa ameuawa katika chumba pamoja na madam Bernadetha ni Joseph Tshibanga.”

“Joseph naye ameuawa? Alishangaa Charles. Wote ndani ya kile chumba walipatwa na mshituko. Hawakutegemea.

“Ndiyo mkuu. Joseph pia ameuawa.”

“Nini walikuwa wanafanya ndani ya nyumba hiyo? Aliuliza mjumbe mwingine wa kikao kile.

“Katika yumba ile ndimo alikuwa amefungwa Gosu Gosu yule mtu ambaye alitumwa Arusha kufanya mauaji. Nadhani walifika pale

ili kuzungumza naye baada ya maelekezo aliyoyatoa Gosu GOsu kuhusu mahali aliko Mathew Mulumbi kutoleta matokeo”

“Gosu Gosu, where is he now? Ni miongoni mwa waliouawa?Aliuliza Charles.

“Gosu Gosu si miongoni mwa waliouawa. Ametoweka na hadi sasa hajulikani mahali alipo. Tunahisi anahusika katika mauaji hayo” alisema Dominic.

“Oh my God ! alisema Charles na kuinamisha kichwa akafikiri kwa muda.

“Julius Mukoke wewe ndiye unahusika na masuala yote ya kiusalama, umekwisha chukua hatua zozote katika kumtafuta huyu Gosu Gosu aliyefanya mauaji haya ya kikatili? Yule mtu anafahamu mambo mengi. Ni mtu hatari sana kwetu” alisema Charles.

“Kuna hatua tayari nimekwisha zichukua tangu nilipoipata taarifa hii. Kwanza kabisa napenda niwajulishe

kuwa nimepokea taarifa kutoka Asset 12. Amenijulisha kuwa Mathew Mulumbi ambaye tunamsaka alifika nyumbani kwa Gavana mara tatu usiku huu. Mara ya kwanza alizungumza na Gavana peke yake. Mara ya pili alirudi akazungumza na Gavana pamoja na Faraji Dilele. Huyu kama mnamkumbuka ni mkurugenzi wa zamani wa SNSA. Anafahamu mambo mengi. Asset 12 aliendelea kunihabarisha kuwa baada ya mazungumzo hayo, Mathew

Mulumbi na Faraji waliondoka wakitumia gari la Mathew. Hakujua walikwenda wapi lakini baadaye walirejea tena Faraji akachukua gari lake alililoliacha pale kwa Gavana akaondoka. Ninaamini mashirikiano hayo ya Gavana, Faraji Dilele na Mathew Mulumbi yana mahusiano na haya mauaji yaliyotokea. Baada ya kuligundua hilo nimetuma vijana wangu kumteka Gavana alfajiri hii wakati akielekea kanisani. Nilipokaribia kufika hapa nilipokea ujumbe kutoka kwa

vijana wangu ambao wamenijulisha kuwa tayari Gavana wamemchukua. Amepelekwa katika level 1 safe house ambako atahojiwa na kueleza kila kitu. Hiyo ni hatua ya kwanza ambayo nimeichukua. Nitaendelea kuwajulisha kila hatua nitakayoichukua.” alisema Julius. Ukimya wa sekunde chache ulitawala ndani ya chumba kile kisha mwenyekiti akasema.

“Kazi nzuri sana Julius umeifanya. Hongera kwa kuchukua hatua za haraka bila

kuchelewa. Binafsi nimefurahi sana kwa hiki ulichokifanya. Nimeshitushwa vile vile kusikia mashirikiano hayo ya Gavana, Fraji na Mathew Mulumbi. Huyu Mulumbi ni mtu ambaye tunamtafuta sana. Ninaamini baada ya kuwa tumempata Gavana, tutafahamu mahali alipo. Hata hivyo umakini mkubwa sana unatakiwa katika jambo hili. Mara tu jua litakapochomoza taarifa za kutekwa kwa Gavana zitaanza kusambaa. Wananchi wataitaka serikali kufanya uchunguzi wa kina kumpata

Gavana. Inatakiwa ahojiwe mapema sana na akishatueleza kile tunachokihitaji basi auawe mara moja”

“Kumuua? Alishangaa Dominic

“Ndiyo. Hapaswi kuendelea kuwa hai. Huyu tayari ni hatari kwetu. Pale atakapotusaidia kumpata Mathew Mulumbi hatakuwa na umuhimu tena kwetu. Kitakachofuata ni kumuua tu. Akiendelea kubaki hai atatusababishia matatizo makubwa.” Alisema Charles.

“Mwenyekiti, suala la kumuua Gavana bado siliafiki. Ninalikataa kwa sababu makubaliano yangu na *Asset 12* ambaye ni mke wake, ni kutomumiza au kumuua Gavana. Bado anampenda. Tukimuua tutakuwa tumekwenda kinyume na makubaliano yetu. Tutamuudhi na anaweza akafanya chochote kibaya kwetu” alisema Julius.

“Julius, anachokizungumza mwenyekiti mimi ninakiafiki. Baada ya kupata kile

tunachokihitaji kutoka kwa Gavana hatakuwa na faida tena kwetu. Kama tayari ameshirikiana na Mathew Mulumbi adui yetu namba moja huyu naye tayari amekuwa ni adui yetu. Lazima naye auawe" aliongeza mjumbe mwingine.

Mjadala uliibuka kuhusu kumuua Gavana. Ililazimu mwenyekiti wa kikao kile kuingilia kati mjadala ule.

"Jua linakaribia kuchomoza na wengine tunahitajika katika shughuli

zetu mbali mbali hivyo tuokoe muda. Suala la kumuua Gavana halihitaji ubishi. Gavana lazima auae lakini baada ya kutusaidia kumpata Mathew Mulumbi. Nina uhakika mkubwa tukimpata Mathew tutawapata pia Gosu Gosu na Regina. Kulipa uzito mkubwa suala hilo, nataka achukuliwe pia Faraji Dilele tena achukuliwe asubuhi hii. Tuma vijana wako wakamchukue ili naye ahojiwe kama Gavana, tuifahamu mipango yao na wapi alipo Mathew. Baada ya kufanikiwa

kupata taarifa tunazohitaji wote wanatakiwa kuuawa” alisema Charles.

“Mwenyekiti bado ninaliona suala hili lina mgogoro mkubwa mbele yake. Kumuua Gavana ni kukosa shukrani kwa mke wake aliyetusaidia kupata taarifa hii muhimu. Bila yeye tusingefahamu kama Mathew na Gavana wanashirikiana” Alisema Julius.

“Julius, hakuna mbadala wa kifo kwa Gavana. Huyu akiendelea kubaki hai ni mtu

hatari sana kwetu. Lazima auawe yeye na washirika wake wote. Misheni yetu tayari imeingia kirusi ambacho lazima tukiondoe kwa gharama zozote zile. Lazima tukiondoe kikwazo chochote kile kinachokuja mbele yetu. Kama unadhani mke wa Gavana anaweza akawa kikwazo kwetu baada ya kumuua mume wake, naye pia aondolewe. Hakuna kumuonea huruma mtu yeyote ambaye ni hatari kwa operesheni yetu.Kumbukeni tayari siri zetu zimevuja na sasa wapo

watu wasiotakiwa kuzifahamu, wamefahamu mipango yetu.Hawa ni kuwaondoa haraka sana” alisema mwenyekiti. Ukimya mfupi ulipita.

“Kuna yeyote mwenye swali kabla sijafunga kikao hiki asubuhi hii? Aliuliza mwenyekiti lakini hakuna aliyeuliza swali.

“Hakuna mwenye swali. Ninakifunga kikao hiki tutakutana saa moja jioni ya leo kwa kikao kingine kirefu zaidi na tutapata taarifa kwa

kina zaidi. Julius kikao cha jioni ya leo kitakuwa kizito kwani tutakuwa na viongozi wakuu hivyo basi hakikisha unakuja na taarifa nzuri kuhusiana na haya yaliyotokea na hatua zilizochukuliwa.” Mwenyekiti alifunga kikao kile. Wajumbe walimpa pole Perfect kwa msiba uliompata kisha wakatawanyika.

****

“Gosu Gosu kwa nini hukunijulisha kama unashirikiana na mtandao hatari? Aliuliza Mathew wakiwa garini muda mfupi baada ya kuondoka katika makazi yao wakielekea nyumbani kwa Faraji Dilele. Gosu Gosu hakujibu alibaki kimya.NI wazi alikuwa analitafuta jibu la kumpa Mathew Mulumbi.

“Mimi, wewe na Ruby tunaishi kindugu. Kanuni yetu kuu ni uwazi. Kwa nini

ukatuficha kuhusu mtandao huu wa siri tena wenye kubeba ajenda za mabeberu? Don't you trust us anymore? Umechoka kuishi Tanzania sasa unataka kurudi Congo? Aliuliza Mathew. Gosu Gosu bado alishindwa kutoa jibu. Aliinamisha kichwa akazama katika tafakari.

"Answer me Gosu Gosu" alisema Mathew.

"Mathew naomba unisamehe ndugu yangu kwa hili nililolifanya" alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu suala si kukusamehe. Ninachotaka kukifahamu kwa nini ukajihusisha na mtandao huu hatari tena kwa kificho? Unafahamu fika watu hawa wanatumiwa na mabeberu katika kufanikisha malengo yao. Wanataka kuwaweka madarakani watu wao ambao watawasaidia katika uporaji wa rasilimali zetu. Hukuliona hilo wakati unakubali kujiunga na mtandao huo? Aliuliza Mathew.

“Mathew nilijaribu sana kutaka kukujulisha juu ya

jambo hili. Nilishindwa nitaanzia wapi kukueleza.” Alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu nataka jibu, nini hasa dhumuni la kujiunga na mtandao huu? Nini unakitafuta? Mathew aliuliza.

“Mathew sina hakika na ninachokitafuta katika mtandao huu. Nahisi hawa jamaa walioniingiza katika mtandao wao walitumia dawa kunishawishi nikajiunga nao.”

“Nani waliokushawishi ukaingia katika mtandao huu?

“Nilikutana na Joseph Tshibanga wakati Rais wa Congo alipofanya ziara ya kikazi hapa nchini. Joseph wakati huo alikuwa mmoja wa wanausalama wa Rais wa Congo. Nilishituka kuonana naye kwa sababu Joseph nilikuwa naye msituni. Kwa kuwa alikuwa tayari na elimu aliondolewa na sikuwahi kumuona tena msituni hadi niliokutana naye hapa Dar es salaam. Baada ya kumdadisi sana ndipo aliponieleza kuwa alipoondoka msituni

alipelekwa kusoma katika nchi mbali mbali.”

“Nani walimpeleka huko nchi za nje kusoma? Aliuliza Mathew.

“Wale wale wanaofadhili makundi ya waasi kwa ajili ya kupambana na serikali. Joseph alipelekwa kusoma kwa manufaa ya mabeberu. Alipachikwa katika serikali lakini alifukuzwa kazi baada ya kufahamika kuwa ni kibaraka wa mabeberu. Alikimbilia Tanzania ambako amekuwa akisimamia misheni ya Congo

mpya. Walinishawishi nijiunge nao kwa ahadi ya kupewa nafasi ya juu ndani ya serikali itakayoundwa baada ya Jenerali Mamba kuondolewa madarakani. Nililazimika kukubali kwani endapo ningekataa wangeniua kwa sababu tayari nimefahamu siri yao.”

“Walikupa majukumu yapi? Mathew aliuliza

“Niliambiwa nisubiri nitapangiwa majukumu lakini hadi jana ndipo nilipofahamu kuwa mauaji niliyoyafanya

kule Arusha ni moja ya majukumu yangu ingawa waliamua kuzunguka njia ndefu kwa kumtumia Ambola kwa sababu wangenifuata moja kwa moja nisingekuali kufanya mauaji yale.” Alisema Gosu Gosu kikapita kimya kifupi.

“Pole kwa yote uliyopitia lakini kama ungenitaarifu mapema kuhusu jambo hili tungekwisha limaliza muda mrefu. Naomba jambo kama hili lisijirudie tena. Uwazi ni kitu muhimu mno.” Alisema Mathew.

“Nimejifunza Mathew. Jambo hili haliwezi kutokea tena.”

“Good.”Alisema Mathew na ukimya ukatawala garini.

“Baada ya kuonana tena na Ambola, mmekwisha yaweka sawa mambo yenu? Aliuliza Mathew.

“Hakuna kinachoendelea tena kati yetu. It’s over. Baada ya kumfahamu Ambola niligundua kumbe mapenzi yote aliyonionesha ilikuwa ni maigizo. Alikuwa kazini. Kwa kuwa nimelifahamu hilo sina

mpango tena wa kuendelea naye. Kila mmoja ataendelea na maisha yake.” Alisema Gosu Gosu.

“Una hakika hutaki tena kuendelea na mahusiano naye? Mathew aliuliza.

“Mathew unanifahamu vyema. Nikisema mambo yamefika mwisho ninamaanisha. Kwa sasa sihitaji tena kuwa na mpenzi. Nina bahati mbaya sana katika upande huo. Kila mahusiano ninayojaribu kuyajenga yamekuwa yananiacha katika

maumivu makali. Sitaki tena. Mambo hayo nitawaachia ninyi. Kwa sasa mipango yangu ni kufanya kazi kwa bidii kutafuta pesa."

"Gosu Gosu usijilaumu wala usijione una bahati mbaya katika mapenzi. Usichoke kutafuta hadi pale utakapompata mtu sahihi kwako. Ninaamini kabisa yupo mtu sahihi kwako na siku moja utampata"

"Mathew sihitaji tena mahusiano yoyote. Nitaishi kama nilivyoishi msit…. ."

Gosu Gosu alinyamaza baada ya ujumbe mfupi kuingia katika simu ya Ruby ambao Mathew aliichukua kwa ajili ya kuwasiliana na Faraji Dilele.

“Tutayazungumza hayo baadaye kwa sasa tujielekeze katika kazi inayotukabili. Soma huo ujumbe unasemaje” Alisema Mathew.

Ujumbe kutoka kwa Faraji uliwaelekeza akina Mathew kuwa tayari amekisha toka ndani ya nyumba yake na amejificha katika gofu lililoko mtaa wa pili kutoka ilipo

nyumba yake. Aliwapa maelekezo akina Mathew namna ya kuweza kufika mahali alipojificha.

“Alifanya vyema kutujulisha kuhusu hao watu waliomfuata kwake. Mathew unaamini watu hao ni kundi moja na wale waliomteka Gavana?” aliuliza Gosu Gosu.

“Ninalazimika kuamini ni kundi moja hasa kutokana na muda ambao ametekwa Gavana na muda ambao watu hao wamefika kuonana na Faraji. Muda unakaribiana

sana. Nimekutana na Faraji na Gavana usiku wa kuamkia leo, nahisi hawa jamaa tayari wamelifahamu ndiyo maana wanataka kumchukua na Faraji pia ili wawahoji waeleze mahali nilipo. Naamini waliofanya kitendo hicho ni mtandao wa akina Bernadetha ambao tayari tumekuwa hatari kwao. Wanajitahidi kututafuta kwa kutumia nguvu zote walizonazo. Swali linalokula akili yangu hivi sasa ni namna walivyofahamu kama nimekutana na Gavana na Faraji jana usiku. Ninauliza

hivyo kwa sababu Gavana alipompigia simu Faraji hakutumia simu yake bali ya mke wake. Je wanafuatilia mawasiliano ya Faraji na Gavana? Kama ndiyo kwa nini? Kuna kitu tunahitaji kukifahamu katika tukio hili la kutekwa kwa Gavana. Ngoja kwanza tukamuokoe Faraji halafu tutajua nini kinachoendelea" alisema Mathew.

"Mathew unamuamini Ambola? Hawezi akatuuza kwa mtanda wao? Aliuliza Gosu Gosu.

“Nimemsikiliza Ambola kwa makini. Nilimtazama machoni wakati akizungumza.Alimaanisha alichokisema. Hawezi akatusaliti”

“C’mon Mathew. Yule mwanamke ni hatari sana. Ni Nyoka mwenye sumu kali. Hapaswi kuaminiwa hata kidogo. Kwa nini tusimfanyie uchunguzi? Kwa nini tusimuwekee mtego tukafahamu nyendo zake? Mathew aliuliza.

“Ambola hana sababu ya kutudanganya. Anatutegemea sisi kuifanya kazi ambayo aliachiwa na baba yake. Najua humuamini tena lakini naomba ujitahidi kumuamini ili misheni yetu ikamilike.” Alisema Mathew. Kimya kilitawala halafu Gosu Gosu akauliza.

“Vipi kuhusu yule mwanamke aliyekuwa naye, Jacline. Hatumfahamu. Ni mara ya kwanza anakutana nasi na amezifahamu siri zetu. Mathew huoni kama tunajiweka katika hatari?

“Gosu Gosu, moja ya sifa yangu kubwa ni uwezo wa juu wa kumsoma mtu na kumfahamu tabia yake hata kama simfahamu. Nimemsoma Jackline hana tatizo. Anaweza akatufaa sana katika misheni hii.”

“Mathew japokuwa unakiri huoni tatizo kwake lakini nitamfuatilia kwa ukaribu sana. Hii dunia imejaa wasaliti. Watu pekee ninaowaamini ni wewe na Ruby. Hawa wengine wote hawatakwepa jicho langu. Nitakapogundua kuna yeyote

anatusaliti I swear nitamjaza risasi katika kichwa chake.” Alisema Gosu Gosu. Mathew hakumjibu kitu alikuwa makini katika usukani.

“Yule jamaa Thomas Ngalula mmewahi kuonana? Mathew aliuliza

“Kabla ya usiku wa kuamkia jana sijawahi kuonana naye. Mtandao huu una watu wengi na wengine wamejificha kama Thomas. He’s good. Anafahamu anachokifanya. Ninamshukuru kwa kunioka ila kitu kimoja tu

kinachoniuma ni kifo cha Bernadetha. Mwanamke yule ni shetani kabisa ninalaumu kwa nini afe kifo chepesi namna ile? Nilipanga kumuua kifo kibaya mno lakini Joseph aliniwahi akamuua." Alisema Gosu Gosu.

"Gosu Gosu kuna kitu ambacho nataka ukifahamu. Kwa kuwa Regina anahisi wanaotaka kumuua ni chama chake, tuliamua kuanza uchunguzi kuwafahamu viongozi wake kiundani. Nilipooneshwa mwenyekiti wa chama cha ukombzi wa Afrika

nilishituka sana kwa sababu ni mtu ninayemfahamu. Anaitwa Israel Maungwana lakini jina lake halisi ni Hammar Perezi. Niliwahi kufanya naye kazi katika shirika la ujasusi Tanzania wakati huo nikiwa mkuu wa kitengo cha kupambana na ugaidi." Mathew alimueleza Gosu Gosu kila kitu kilichotokea hadi familia yake ilivyoteketezwa katika moto.

"Israel Maungwana ndiye aliyeidhinisha familia yangu iteketezwe. Kama si mkurugenzi wangu kuniokoa

hata mimi hivi sasa ningekwisha uawa. Ni mtu hatari sana. Anashirikiana na mtu mwingine hatari anaitwa Diana Watvon. Hawa ni watu hatari kabisa kwa nchi. Ni watu wanaotumiwa na nchi kubwa kutengeneza migogoro mikubwa barani Afrika kwa maslahi ya mabeberu. Hiki chama cha ukombozi wa Afrika ni chama kilichojaa vibaraka wa mabeberu. Wanatekeleza ajenda za mabeberu ambao mate huwatoka kwa utajiri mkubwa uliopo nchini kwetu na katika bara la Afrika.

Chama hiki na mtandao wao wote wameotesha mizizi hadi ndani ya serikali ndiyo maana wana uhakika mkubwa wa mipango yao yote ya hujuma za uchaguzi kufanikiwa. Sisi tunatakiwa kusimama imara na kuhakikisha mipango yao yote haifanikiwi. Tunapaswa kulipigania taifa letu dhidi ya mabeberu.” Alisema Mathew.

“Mathew pole sana. Hukuwahi kunieleza kuhusu kuteketezwa kwa familia yako” alisema Gosu Gosu.

“Si suala ambalo hupenda kulizungumzia. Huwa linaniumiza sana.”

“Kwa nini tusifanye mpango akapatikana huyo Israel akalipa uovu wake? Mimi niko tayari kumtafuta kokote aliko. Siogopi kama ni mtu hatari au vpi. Nitaingia kokote kule kumsaka hadi nihakikishe anapatikana” alisema Gosu Gosu.

“Nchi kwanza. Gosu Gosu kwa sasa tuna majukumu makubwa ya kuhakikisha nchi yetu inabaki salama.

Tujielekeze katika misheni hiyo. Pale tutakapohakikisha mipango yao imevurugwa basi utabaki uwanja wa mimi na Hammar. Sintopenda kumshirikisha mtu mwingine katika jambo hili. I'll do it my way" alisema Mathew.

"Mathew mimi ni ndugu yako. Sintakuacha ukamuadhibu bazazi huyo peke yako. Nitakwenda nawe. Nitamuondoa kiungo kimoja baada ya kingine."

"Gosu Gosu tunaukaribia mtaa anakoishi Faraji.

Muandikie Faraji ujumbe kuwa tumekaribia sana kufika mahali alipo” alielekeza Mathew na Gosu Gosu alimuandikia Faraji ujumbe kama alivyoelekezwa.

Waliupita mtaa ule anakoishi Faraji Dilele wakaingia katika mtaa wa pili ambako kwa maelekezo aliyowapa akina Mathew ndiko alikojificha. Waliyafuata maelekezo waliyopewa, walikivuka chuo cha utalii, wakalivuka shamba kubwa la kiwanda cha maziwa ambamo mamia ya Ng’ombe walikuwa

wanachungwa. Shamba lilizungushiwa uzio wa seng'enge. Mita kadhaa kutoka katika shamba lile kulikuwa na jengo la kiwanda lililozungushiwa ukuta lakini kiwanda hicho bado hakikuwa kimeanza uzalishaji. Kutoka kiwandani hapo kulikuwa na eneo la mita mia mbili likiwa wazi. Mbele ya eneo hilo la wazi ndipo kulikuwa na jengo chakavu la ghorofa tano ambalo lilionekana kujengwa miaka mingi bila kumaliziwa.

"Kwa mujibu wa maelekezo aliyoyatoa Faraji,

amejificha katika lile jengo pale.” Mathew alisema huku akipunguza mwendo na kusimamisha gari mita kadhaa kabla ya kulifikia lile jengo. Alitoa bastola yake akaishika mkononi. Gosu Gosu naye alifanya hivyo.

“Mpigie Faraji mjulishe atoke nje aje garini” alisema Mathew huku akiufungua mlango akashuka. Gosu Gosu naye aliufungua mlango akashuka huku simu ikiwa sikioni. Mathew aliegemea gari huku macho akiwa ameyaelekeza katika jengo lile.

“Simu yake inaita bila kupokelewa” alisema Gosu Gosu.

“Piga tena” alisema Mathew. Gosu Gosu alipiga tena lakini simu haikupokelewa.

“Simu haipokelewi” alisema Gosu Gosu.

“Kwa nini hapokei simu wakati alidai amejificha katika jengo hili? Aliuliza Mathew huku akiendelea kulikazia macho jengo lile. Mara ujumbe wa simu uliingia.

“Zunguka nyuma ya jengo kuna gari nimejificha humo” ulisomeka ujumbe huo.

“Kwa nini anaogopa kujitokeza wakati tayari tumekwisha fika? Aliuliza Mathew ambaye alionesha wasi wasi.

“Mathew tumfuate huko huko mahali alikojificha” alisema Gosu Gosu kisha kwa tahadhari walitembea kulizunguka jengo lile.

“Jengo zuri sana hili . Kwa nini limetelekezwa? Aliuliza Gosu Gosu lakini Mathew

hakumjibu alikuwa makini jicho lake likizunguka kama Kinyonga.

Hakukuwa na dalili zozote za kuwepo mtu katika jengo lile. Walizunguka upande wa nyuma ambako kama ujumbe ule ulivyoelekeza kulikuwa na gari dogo lenye rangi ya fedha. Walilisogelea gari lile kwa tahadhari kubwa. Gari lilikuwa na vioo vyeusi kiasi cha kutomuwezesha aliye nje kuona ndani. Mathew aliusogelea mlango akagonga. Wakati wakisubiri mlango wa

gari ufunguliwe, ghafla ilisikika sauti kali.

“Hivyo hivyo mlivyo inueni mikono juu iwekeni nyuma ya vichwa vyenu.!

Sauti ile kali iliwafanya Mathew na Gosu Gosu kuinua vichwa vyao na kumshuhudia jamaa mmoja akiwa amesimama katika dirisha ghorofa ya pili akiwa na bunduki. Mara nyuma yao walitokea watu watatu wote wakiwa na bastola wamezielekeza kwa akina

Mathew. Walizingirwa kila kona.

“Taratibu pigeni magoti. Msitoe mikono nyuma ya vichwa vyenu ! aliamuru yule jamaa aliyekuwa ghorofani ambaye baada ya Mathew kumtazama vyema alikuwa na jicho moja tu la kulia.

“Wewe ni nani na unafanya nini hapa? Mathew aliuliza lakini badala ya kujibiwa ilimkosa risasi na kupiga gari. Jamaa yule mwenye jicho moja hakuwa na masihara hata kidogo.

Mathew na Gosu Gosu walipiga magoti kama walivyoamriwa. Jamaa wawili waliokuwa nyuma ya akina Mathew waliwasogelea huku wakiwa katika tahadhari kubwa.

“Wakagueni, chukueni silaha kisha wafungeni pingu haraka sana! Aliamuru yule jamaa ghorofani huku akiwa makini kuhakikisha hakuna tatizo lolote linajitokeza.

Jamaa mmoja aliushika mkono wa kulia wa Mathew kwa lengo la kuufunga pingu

lakini kabla hajaichomeka pingu ile katika mkono, Mathew alisimama kwa kasi ya ajabu akamgeuza yule jamaa akamkaba kabali nzito na kwa kutumia mkono wake wa kushoto aliichomoa bastola ya yule jamaa iliyokuwa kiunoni. Jicho la Mathew lilizunguka kama la Kinyonga na kabla hajaizinga ile bastola alikiona kidole cha yule jamaa ghorofani tayari kikiwa katika kizinga. Alimsukuma yule jamaa aliyekuwa amemkaba halafu kama kima akaruka pembeni. Milio ya risasi

ilisikika. Jicho moja alikuwa ameachia risasi lakini kwa bahati mbaya hazikumpata Mathew ambaye aliwahi kuruka, zikampata yule mwenzake. Jicho moja alipatwa na mshangao baada ya kumuona mwenzake akianguka chini huku akivuja damu mwilini. Mathew hakumkawiza aliiachia risasi mbili kutoka katika bastola ya yule jamaa aliyokuwa ameishika mkononi ambazo zilimpata jicho moja akaangukia ndani huku

bunduki aliyokuwa ameishika ikianguikia nje.

Mathew na Gosu Gosu ni kama vile walikuwa wameambizana nini cha kufanya. Wakati Mathew alipomgeuza yule jamaa aliyetaka kumfunga pingu na kumkaba kabali, Gosu Gosu naye aligeuka bila hofu na kumtandika teke zito sehemu za siri jamaa aliyekuwa nyuma yake akiwa na pingu tayari kumfunga. Uzito wa teke lile ulimfanya jamaa achuchumae kwani alihisi korodani zake zimepasuka. Kwa kasi ya aina

yake Gosu Gosu aliichomoa bastola yake yenye kiwambo cha sauti akamlenga jamaa aliyebaki ambaye aligeuka na kuanza kukimbia. Risasi mbili zilitosha kumuondoa uhai yule jamaa. Gosu Gosu hakusumbuka kumuangalia kama amekufa, alimfuata yule jamaa aliyekuwa anagala gala chini kwa maumivu baada ya kutandikwa teke. Akiwa na hasira mithili ya Mbogo aliyejeruhiwa, hakupoteza muda alimtandika risasi mbili jamaa akakata pumzi.

“Usingemuua huyo ili atusaidie kupata taarifa nani kawatuma? alisema Mathew.

“Samahani Mathew. Nina hasira mno na hawa washenzi ndiyo maana sikutaka kumpa nafasi” alisema Gosu Gosu.

“Hakuna tatizo. Tujiridhishe kwanza kama walik……” Mathew alinyamaza baada ya gari lile kuanza kutikisika. Taratibu walilisogelea. Mathew alipiga teke kioo cha dirisha akachungulia ndani. Hakukuwa na mtu. Haraka

haraka alifungua buti na kumkuta Faraji Dilele akiwa amefungwa mikono na miguu kwa kamba. Mdomoni alifungwa kitambaa ili asiweze kutoa sauti. Alikuwa na majeraha sehemu mbali mbali za mwili wake. Mathew alimtoa akamfungua zile kamba na kumtoa kile kitambaa alichofungwa mdomoni.

“Mathew Mu……ah ! Faraji alitaka kusema kitu akashindwa. Mathew alimuinua akamuweka begani.

“Tuondoke mahali hapa! Alisema Mathew wakaanza kupiga hatua wakiwa katika tahadhari kubwa kuelekea katika gari lao. Mlango ulifunguliwa wakamuingiza Faraji ndani ya gari wakaondoka kwa kasi.

“Ma. . Ma. . Mathew , my family” alisema Faraji.

“Faraji kipaumbele cha kwanza ni wewe uwe salama kwanza. Tunakuondoa kwanza wewe katika eneo hili la hatari. Familia yako usihofu

watakuwa salama.” Alisema Mathew.

****

“Ninawashukuru sana Mathew kwa kuniokoa kutoka katika mikono ya wale jamaa. Nilikwisha yakabidhi maisha yangu kwa Mungu nikijua mwisho wangu umefika. Sikuwa na mategemeo ya kutoka salama katika mikono wale maharamia.” Alisema Faraji baada ya kufikishwa katika kambi ya akina Mathew na kugangwa majeraha yake.

“likuaje ukashindwa kutoka nyumbani kwako hadi jamaa wakakupata? Mathew aliuliza.

“Nilishindwa kutoka ndani kwa kutumia mlango wa nyuma kama mlivyonishauri. Nilichelewa. Nilipotoka tu ndani ya chumba changu ili niondoke, niliwakuta jamaa wawili tayari wamesimama nje ya mlango wangu. Waliniweka chini ya ulinzi, wakanichukua wakaniweka katika gari lao wakanipeleka katika lile jumba bovu. Waliichukua simu yangu wakaanza kuwasiliana nanyi

kwa kutumia ujumbe mfupi wa simu wakawaelekeza mje katika jengo lile. Walinifunga kamba wakaniweka ndani ya buti sikujua kilichoendelea tena hadi pale niliposikia milio ya risasi halafu nikasikia watu wakizungumza. Niliitambua sauti yako ndiyo maana nilianza kugonga gari kwa miguu ili mfahamu nilikuwa ndani ya gari. Ahsanteni sana kwa kuniokoa. Hofu yangu kwa sasa ni kwa familia yangu.” alisema Faraji.

“Faraji kwa sasa unatakiwa uhofie maisha yako. Familia

yako watakuwa salama. Hawa jamaa hawana shida na familia yako wanayekuhitaji ni wewe pekee.” Alisema Mathew.

“Mathew hawa jamaa wakinikosa, lazima watailenga familia yangu.”

“Faraji, usalama wa familia yako ni kutokujua mahali ulipo. Pindi wakifahamu mahali ulipo basi watakuwa katika hatari kubwa. Kuanzia sasa hautawasiliana nao hadi pale mambo yatakapotulia.” Alisema Mathew.

“Mathew lazima niwajulishe familia yangu kuwa niko salama. Natakiwa niwatoe hofu” alisema Faraji.

“Faraji nisikilize. Familia yako watakapofahamu kuwa uko salama hiyo itakuwa ni tiketi yao ya kifo. Ni vyema mambo yakabaki kama yalivyo hivi sasa yaani wsifahamu chochote kuhusiana na mahali ulipo. Tukiliweka kando hilo nataka kujua wale jamaa kuna kitu chochote walikuuliza?

“Hawakuniuliza chochote. Walichokifanya baada ya

kunikamata walichukua simu yangu wakaipekua wakaipata namba ya mwisho niliyowasiliana nayo ambayo niliihifadhi kwa jina la Mathew. Waliniuliza ni Mathew yupi niliyekuwa nawasiliana naye sikuwajibu ndipo walipoanza kuwasiliana nanyi kwa kutumia ujumbe mfupi. Nilifanya kosa kubwa kuhifadhi namba ile kwa jina la Mathew. Nilihatarisha maisha yenu" alisema Faraji.

"Usijali. Hakuna aliyetegemea kama mambo

yangefika hapa yalipofika.” Alisema Mathew.

“Mathew mnadhani matuko haya ya kutekwa Gavana na mimi, yanahusiana na kile tulichokifanya usiku wa kuamkia leo? Aliuliza Faraji.

“Ndiyo. Tunaamini sababu kuu ya kutekwa kwa Gavana ni makutano yetu jana usiku. Wale jamaa tayari wamefahamu japo sijui wamefahamu vipi. Wananitafuta mimi kwa udi na uvumba. Wana hofu kubwa kwa kuwa tayari ninaifahamu

mipango yao. Mimi ni kirusi kwao hivyo lazima wahakikishe wanakiondoa kirusi hicho kwa gharama zozote zile. Baada ya kufahamu nimekutana nanyi, waliona njia pekee ya kujua mahali nilipo ni kwa kuwateka wewe na Gavana. Ninakuahidi lazima tutamtafuta Gavana na kumpata.” Alisema Mathew.

“Mathew swali la namna hawa jamaa walivyofahamu kama tulikutana jana usiku, linaniumiza kichwa sana. Walifahamuje? Aliuliza Faraji.

“Bado hatujui ni namna gani walifahamu. Tunalifanyia kazi hilo. Kuna mambo mengine pia yametokea usiku wa kuamkia leo” Mathew alimweleza Faraji kile kilichotokea usiku namna Gosu Gosu alivyokombolewa.

“Mathew, mwili umenisisimka sana kwa haya uliyonieleza. Ni mambo mazito. Sikutegemea kama jambo hili ni kubwa kiasi hiki.”

“Ni jambo kubwa. Huu ni mtandao mkubwa wenye nguvu uliojiandaa kufanya kitu

chochote ili kuhakikisha mipango yao inafanikiwa. Hawataki kikwazo chochote katika njia wanayopita. Pamoja na hayo hatuogopi. Tutapambana nao hadi tuhakikishe mipango yao yote inavurugwa” alisema Mathew bila hofu yoyote.

“Mathew nimeingiwa na hofu kubwa. Najiona kama siko salama hata kidogo. Hawa jamaa hawatashindwa kunitafuta na kujua niko hapa.Nitawaweka pia ninyi katika hatari kubwa.Nahitaji kuwa mbali na ninyi kwa sasa

ili muweze kuifanya kazi yenu kwa salama.Sitaki vile vile kuwaongezea mzigo wa kunilinda” alisema Faraji.

“Hapa ni sehemu salama kwa wewe kuwepo. Au una sehemu nyingine ambako unadhani ni salama zaidi kwako? Aliuliza Mathew. Faraji alifikiri kidogo na kujibu.

“Nina mwanangu anaitwa Musa Faraji. Anafanya kazi SNSA. Nadhani kwake ninaweza kuwa salama”

alisema Faraji, Mathew alipatwa na mshangao.

“Nilikuuliza mbele ya Gavana kama kuna mtu yeyote ndani ya SNSA anayeweza kutusaida hukusema kama una mtoto wako anafanya kazi SNSA” alisema Mathew.

“Ni mtoto niliyemzaa nje ya ndoa. Familia yangu hawajui kama nina mtoto nje ya ndoa.”

“Hakijaharibika kitu. Unamuamini anaweza akakulinda?

“Ndiyo. NIkifanikiwa kuzungumza naye lazima atanisaidia”

“Good. Tutawasiliana naye. Huyu anaweza pia akatusaidia sana katika mambo mengi ndani ya SNSA”

“Mathew naomba msimshirikishe mwanangu katika jambo hili. Mtayaweka maisha yake hatarini”

“Faraji hatuna namna, lazima tumshirikishe mwanao. Idara ya SNSA ambayo dhumuni lake ni ulinzi wa taifa, imebadilishwa matumizi

na sasa inatumika kutekeleza ajenda za mabeberu. Kuna mambo mengi ninaamini tutayapata kama tukiwa na mtu ndani ya SNSA. Tupe namba yake tuwasiliane naye" alisema Mathew. Faraji alisita kidogo halafu akataja namba ya simu ya mwanaye.

"Ruby mpigie simu huyu jamaa tuzungumze naye" alisema Mathew. Ruby hakupoteza muda alimpigia simu Musa ikapokelewa.

"Hallow"ilisema sauti upande wa pili wa simu.

“Hallow nazungumza na Musa Faraji? Aliuliza Mathew.

“Ndiyo. Nani mwenzanu?

“Musa tafadhali naomba unisikilize. Je upo kazini?

“Hapana. Niko nyumbani. Wewe ni nani?

“Musa kuna mtu anahitaji kuzungumza nawe” alisema Mathew na kumpatia Faraji simu azungumze na mwanae.

“Musa hujambo? Aliuliza Faraji.

“Baba?! Musa alishangaa.

“Ndiyo. Hujambo?

“Sijambo baba. Shikamoo”

“Marahaba. Unaendeleaje?

“Ninaendelea vizuri baba. Vipi wewe unaendeleaje?

“Ninaendelea vyema. Musa imekuwa vyema uko nyumbani. Nimekupigia ninaomba msaada wako”

“Msaada?

“Ndiyo. Ninaomba msaada wako. Niko katika hatari.Ninatafutwa na watu nisiowafahamu. Nimefanikiwa kuwatoroka na sina sehemu

nyingine ya kwenda ambako nitakuwa salama. Ninaomba nije nijihifadhi kwako kwa siku kadhaa. Ninaamini hapo nitakuwa salama" alisema Faraji.

"Baba nani wanakutafuta?

"Musa nitakueleza kila kitu nikifika hapo nyumbani kwako."

"Uko wapi nikufuate? Musa aliuliza.

"Usisumbuke tafadhali. Ninakuja hapo sasa hivi" alisema Faraji na kukata simu.

“Hakuna kupoteza muda twende nikupeleke huko kwa mwanao ili tukazungumze naye. Siku ya leo tuna mambo mengi ya kufanya” alisema Mathew na kutoa maelekezo kwa Ruby na Gosu Gosu kwenda nyumbani kwake kuchukua gari maalum ambalo wangelitumia siku ile katika kufanya uchunguzi kwenye msiba wa Bernadetha.

****

Mathew na Faraji walifika katika nyumba anayoishi Musa. Ni nyumba kubwa iliyozungukwa na ukuta mrefu wenye rangi nyeupe. Musa alijulishwa, akatoka na kufungua geti akina Mathew wakaingia ndani. Faraji ndiye aliyekuwa wa kwanza kufungua mlango wa gari akashuka. Musa alishituka baada ya kumuona baba yake akiwa na majeraha sehemu mbali mbali za mwili wake.

“Baba kuna nini? Aliuliza Musa. Mathew aliufungua mlango akashuka.

“Musa twende tukazungumzie ndani tafadhali” alisema Faraji. Musa aliwaongoza hadi ndani. Bado alikuwa katika mshangao mkubwa.

“Musa, huyu niliyeongozana naye anaitwa Mathew Mulumbi.”

“Mulumbi? Musa alishangaa.

“Ndiyo. Unamfahamu?

“Jina hilo si geni masikioni mwangu. Karibu sana brother.”

“Ahsante. Alijibu Mathew.

“Baba nini kimetokea? Nani hao waliokujeruhi namna hii? Aliuliza Musa.

“Musa nadhani umesikia tukio la kutekwa Gavana alfajiri ya leo”

“Ndiyo nimelisikia tukio hilo. Ni tukio la kushangaza sana” alisema Musa.

“Waliomteka Gavana ndio waliotaka kuniteka mimi. Ni

Mathew Mulumbi aliyeniokoa. Bila yeye hivi sasa na mimi ningekuwa mahali kusikojulikana”

“Kuna nini kinaendelea baba hadi wewe na Gavana mtekwe na watu hao? Musa aliuliza.

“Kuna mambo makubwa yanaendelea hapa nchini hivi sana” alisema Mathew na kumtazama Faraji.

“Nakusikiliza kaka” alisema Musa.

Mathew alimweleza Musa kwa kifupi kuhusu tukio la kutaka kumuua Regina jijini Arusha.

“Nililisikia tukio hilo. Lakini lilivyotangazwa ni tofauti na unavyonieleza.” Alisema Musa.

“Ninachokueleza mimi ndiyo ukweli halisi kwani ndiye niliyekuwa eneo la tukio.” Alisema Mathew na kuendelea kumweleza Musa kilichofuata baada ya tukio lile.

Yote aliyoelezwa yalimuacha Musa katika mshangao

mkubwa sana. Yalikuwa ni mambo mageni kwake.

“Nimeshangaa sana kwa haya uliyonieleza. Ni mambo makubwa na mazito.” Alisema Musa.

“Kwa hiyo Musa nimekuja hapa kwako kujihifadhi kwa siku kadhaa wakati Mathew na wenzake wakishughulikia haya mambo aliyokueleza” alisema Faraji.

“Kutakuwa na tatizo lolote kwa baba yako kujihifadhi hapa kwako kwa muda wakati tukiendelea kushughulika na

mtandao huu hatari? Mathew aliuliza.

“Hakuna tatizo lolote. Huyu ni baba yangu. Ni jukumu langu vile vile kuhakikisha kwa namna yoyote ile anakuwa salama. Ataishi hapa kwa muda wote anaouhitaji na atakuwa salama” alijibu Musa.

“Good. Pamoja na hayo kuna kitu kingine tunakihitaji kutoka kwako.” Alisema Mathew.

“Kitu gani brother? Aliuliza Musa.

“Tunahitaji kumpata mtu wa kutusaidia mambo mbali mbali kutoka ndani ya SNSA. Tunaomba tukutumie wewe kila pale tutakapokuwa tunahitaji msaada kutoka ndani ya SNSA” alisema Mathew.

“Mimi niko tayari kuwasaidia lakini kwa sasa niko likizo. Pamoja na hayo kama kuna kitu mnakihitaji mnaweza kuwasiliana nami kwani bado ninaweza kuingia katika mfumo wa SNSA na kufanya chochote au ninaweza kumtumia mmoja wa marafiki

zangu ambaye ameshika nafasi yangu wakati huu nikiwa likizo.”

“Ahsante sana Musa. Tutawasiliana nawe kila pale tutakapokuwa na uhitaji.” Alisema Mathew.

Baada ya mazungumzo ambayo hayakuchukua muda mrefu, aliagana na akina Faraji akaondoka kurejea katika kambi yao.

LEVEL 1 SAFE HOUSE – DAR ES SALAAM.

Mlango wa chumba alimofungwa Gavana Jackson Mzumile ulifunguliwa, wakaingia watu watatu. Gavana ambaye alikuwa anavuja jasho kutoka na chumba kile kuwa na joto kali aliingiwa na hofu kubwa. Watu wawili walisimama wakiuegemea ukuta halafu jamaa mmoja alisogeza kiti karibu na Gavana akaketi. Alimtazama kwa sekunde kadhaa halafu akasema.

“Hallo Gavana Jackson.”

Gavana hakumjibu kitu aliendelea kumtazama kwa hofu. Jamaa yule alikuwa na kovu kubwa chini ya jicho lake likionesha jamaa aliwahi kukatwa na kitu.

“Gavana pole sana kwa usumbufu ulioupata. Muda si mrefu tutakurejesha nyumbani kwako lakini kabla ya kukurejesha kwako, kuna maswali machache tunataka kukuuliza” alisema yule jamaa kwa sauti ya upole jambo lililompa faraja Gavana.

“W. . water” alisema Gavana kwa sauti ya chini. Koo lake lilikauka kutokana na joto kali. Yule jamaa alitoa maelekezo na chupa ya maji ya kunywa ililetwa halafu kiyoyozi kiliwashwa hali ya hewa ndani ya kile chumba ikawa ya ubaridi. Gavana alifunguliwa mikono akanywa maji yote katika ile chupa.

“Mheshimiwa Gavana kuna kitu kingine unahitaji? Chai, Kahawa au mvinyo kama utapenda” alisema yule jamaa.

“Ahsanteni kwa maji. Sihitaji kingine chochote. Nini hasa mnakitaka kwangu? Aliuliza Gavana baada ya kumaliza ile chupa ya maji.

“Kuna mambo machache tunataka kuyafahamu kutoka kwako kisha tutakurejesha nyumbani kwako ukaendelee na majukumu yako kwa taifa” alisema yule jamaa huku akizungusha kidole katika Kishkwambi alichokuwa nacho.

“Nini hasa mnataka kukifahamu? Aliuliza Gavana.

Yalikuwa ni mazungumzo ya kirafiki kabisa. Jamaa alimsogezea Gavana Kishkwambi na kumuuliza.

“Unamfahamu huyo mtu pichani?

Gavana aliitazama ile picha kwa makini. Alipatwa na mshituko mkubwa. Mtu yule ambaye picha yake ilikuwa katika kishkwambi ni Mathew Mulumbi.

“Unamfahamu huyo mtu Gavana? Aliuliza tena yule jamaa.

“Hapana simfahamu” alijibu Gavana.

Yule jamaa alimtazama kwa makini sana.

“Una uhakika Gavana? Aliuliza

“Ndiyo. Simfahamu mtu huyu.”

“Hujawahi kumuona sehemu yoyote?

“Ni mara ya kwanza ninamuona. Ni nani huyu mtu? Anahusiana nini na mimi? Gavana aliuliza. Yule jamaa hakumjibu alichukua

kishkwambi akaitafuta picha nyingine na kumuonesha Gavana.

“Huyu naye unamfahamu? Aliuliza yule jamaa. Licha ya hali ya hewa mle chumbani kubadilika na kuwa ya ubaridi mzuri, matone ya jasho yalionekana katika paji la uso wa Gavana. Picha iliyoonekana katika Kishkwambi ilikuwa ni picha ya Faraji Dilele.

“Mungu wangu. Hawa jamaa tayari wamefahamu kuwa nilikutana na hawa watu wawili usiku wa kuamkia leo.

Wamefahamuje kama nimekutana nao? Mbona makutano yetu yalikuwa ya siri? Hata hivyo nafahamu lengo lao, wanataka nikubali kuwa ninawafahamu hawa watu wawili halafu watanitaka niwaoneshe mahali walipo. Siko tayari Mathew Mulumbi aingie katika mikono ya hawa jamaa. Ni yeye ambaye anapambana kuharibu mipango ya hawa watu. ni yeye ambaye atakuja na majibu wapi alipo mwanangu Kelvin. Mathew ni mtu anayetakiwa kulindwa kwa gharama zozote

zile hata kama itanigharimu uhai wangu” aliwaza Gavana.

“Gavana mbona uko kimya? Unamfahamu huyo mtu pichani? Yule jamaa aliuliza.

Gavana alitikisa kichwa na kusema.

“Hapana simfahamu huyu mtu ni nani”

Jamaa alikichukua kishkwambi chake akairudisha tena picha ya Mathew Mulumbi halafu akampa Gavana.

“ Check again. Itazame tena vizuri picha hii. Jaribu kukumbuka kama umewahi kumuona mahali huyu mtu” alisema yule jamaa.

“Simfahamu huyu mtu hata kama ningemtazama mara elfu moja” alisema Gavana.

“Mheshimiwa Gavana una uhakika humfahamu huyu mtu? Aliuliza tena yule jamaa.

“Hapana simfahamu. Ningewaambia kama ninamfahamu” alijibu Gavana. Yule jamaa alivua miwani

myeusi aliyovaa, akamtazama Gavana. Japokuwa alikuwa anaongea kwa sauti ya upole lakini macho yake yalitisha. Yalikuwa mekundu sana.

“Hawa watu wanaonekana ni makatili sana.” Aliwaza Gavana.

“Gavana nakuuliza kwa mara ya mwisho, hawa watu niliokuonesha picha zao unawafahamu? Aliuliza yule jamaa.

“Vijana wangu, hawa watu siwafahamu.” Alijibu Gavana.

“Una uhakika hujawahi kuonana nao sehemu yoyote?

“Hapana sijawahi kukutana nao. Ni mara ya kwanza ninaona picha zao” alijibu Gavana.

Yule jamaa alivaa miwani yake halafu akachukua kishkwambi na kusimama.

“Ahsante Gavana kwa ushirikiano wako lakini bado unaonekana hutaki kutueleza ukweli. Nitakuacha tena humu ndani kwa muda ili utafakari kuhusu hawa watu niliokuonesha picha zao.

Nataka urudishe kumbu kumbu zako nyuma ukumbuke kama umewahi kukutana na hawa watu. Nitakapokuja tena naamini utakuwa na jibu zuri la kunipa" alisema yule jamaa.

"Vijana wangu ninawaambia ukweli hawa watu siwafahamu. Tafadhali naombeni mniruhusu niondoke hapa kama mlivyoniahidi" alisema Gavana.

"Mheshimiwa Gavana, kuondoka hapa ni wewe utakayeamua. Kama

utachagua kusema ukweli tutakurejesha nyumbani lakini kama utaendelea kudanganya basi utaendeleea kukaa humu ndani. Uchaguzi ni wako Gavana” alisema yule jamaa na kutoa maelekezo Gavana akafungwa pingu.

“Hamuogopi kama jeshi la polisi wananitafuta hivi sasa? Aliuliza Gavana lakini jamaa tayari walikwisha toka nje. Mara kile kiyoyozi kilizimwa na joto likaanza.

“Ee Mungu, kama siku yangu imefika, basi

ninaikabidhi roho yangu katika mikono yako mitakatifu lakini kama bado unanihitaji niendelee kuishi hapa duniani ninakuomba uniondoe katika mateso haya kutoka kwa watu ambao wana malengo mabaya na nchi yetu" Gavana aliomba sala fupi. Tayari alikwisha ziona dalili za kutokutoka salama katika mikono ya wale jamaa. Safari hii joto llikuwa kali zaidi kushinda hata lile la awali.

Baada ya kutoka ndani ya kile chumba yule jamaa aliyekuwa anamuhoji Gavana

alitoa simu yake akalitafuta jina limeandikwa Boss, akapiga.

“Red unasemaje? Aliuliza jamaa aliyepokea simu.

“Boss, nimetoka kumuhoji Gavana lakini hajatoa ushirikiano. Bado tuko katika hatua za awali. Tunaendelea na zoezi la joto. Tumepandisha joto zaidi. Baada ya saa moja tutamuhoji tena kama atakuwa tayari kufunguka” alijibu yule jamaa ambaye alitajwa kwa jina moja la Red.

“Kazi nzuri. Endeleeni hatua kwa hatua lakini kama nilivyowaeleza hatakiwi kuumizwa. Nina uhakika hataweza kuvumilia mateso hayo lazima ataamua kufunguka ataeleza kila kitu. Mkipata chochote cha muhimu mtanijulisha”

“Sawa mkuu” alisema Red na kukata simu akaingia katika chumba kilichokuwa na runinga mbili. Moja ilionesha filamu na nyingine iliyokuwa ukutani ilionesha chumba alimo Gavana Jackson. Jamaa

walimimina mvinyo wakaendelea kunywa taratibu.

****

Mathew alirejea salama katika makazi yao akitokea nyumbani kwa Musa alikompeleka Faraji Dilele.

“Kila kitu kinakwenda vizuri hapa? Aliuliza baada ya kuwakuta akina Gosu Gosu wakiendelea na maandalizi ya gari watakalolitumia watakapokwenda katika msiba wa Bernadetha.

“Hakuna tatizo lolote. Nyumbani kwako ni salama kabisa. Watumishi wako wanadai kuna watu wamekuwa wakifika mara kwa mara nyumbani kwako kukuulizia” alisema Ruby.

Mathew aliwapa mrejesho wa kile alichokipata kutoka kwa Musa mtoto wa Faraji.

Wakati Gosu Gosu na Ruby wakiendelea na maandalizi ya gari, Mathew aliingia ndani moja kwa moja hadi katika chumba cha Jombaa.

“Habari yako Jombaa. Unaendeleaje?

“Ninaendelea vizuri. Nini kinaendelea huko nje? Aliuliza Jombaa.

“Huko bado mambo si shwari. Bado unatafutwa. Usihofu tafadhali hapa utakuwa salama.”

“Mathew sijazoea kukaa ndani namna hii. Unadhani nitakaa ndani hadi lini? Aliuliza Jombaa.

“Kwa sasa sina jibu la kukupa lakini endelea kukaa

hapa hadi pale mambo yatakapotulia. Nimeshaamua kukusaidia hivyo usiwe na wasi wasi nitakusaidia. Ninachohitaji unihakikishie jambo moja tu kwamba pale mambo yatakapomalizika utaachana na mambo yako ya uhalifu na utakuwa raia mwema”

“Mathew, uhalifu ndiyo maisha yangu. Wazazi wangu wote wawili walikuwa wanajihusisha na uhalifu na mimi nimerithi kutoka kwao. Nitaishi vipi kama sintandelea na kazi hii?

“Nitakusaidia kuyaanza maisha mapya. Uhalifu mwisho wake ni mbaya sana. Tazama sasa unatafutwa na jeshi la polisi kwa tuhuma za mauaji. Zile pesa kidogo ambazo unalipwa kwa uhalifu hazikusaidii chochote kwa sasa. Huna sababu yoyote ya kuendelea na mambo hayo. Tafadhali vumilia wakati mimi na wenzangu tunajitahidi kulimaliza suala hili halafu tutakusaidia” alisema Mathew.

“Mathew, kuna swali nimekuwa najiuliza sana ambalo unaweza ukanisaidia

kupata majibu. Kwa nini wale watu wawili kule Arusha walitakiwa kuuawa? Walifanya kosa gani? aliuliza Jombaa. Ilimlazimu Mathew kukaa kitandani.

“Sikiliza Jombaa. Kuna mambo makubwa yanaendelea hapa nchini hivi sasa. Nikipata nafasi nzuri nitakuelezea kila kitu lakini kwa ufupi tu ni kwamba wale watu walitakiwa kuuawa kwa sababu kuna kitu walikifahamu ambacho hawakutakiwa kukifahamu. Ni mambo yanayohusiana na usalama wa nchi.”

“Kitu gani walikifahamu ambacho hawakutakiwa kukifahamu hadi kikawagharimu uhai wao?

“Kuna mtandao wa watu wanaoshirikiana na watu kutoka nje ya nchi ambao lengo lao ni kuharibu uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika hapa nchini hivi karibuni. Wale watu wawili waliotakiwa kuuawa waliifahamu siri hiyo ndiyo maana wakatakiwa kuuawa. Kwa bahati mbaya kwetu na nzuri kwao mtu aliyekuwa na taarifa zote kuhusiana na nini hao jamaa

wamepanga kukifanya ni yule kijana aliyeuawa. Mwanamke ambaye alisalimika naye alikuwa anategemea kupata taarifa kutoka kwa yule jamaa. Kwa sasa hatufahamu ni namna gani wamepanga kufanya hujuma, tunaendelea kuchunguza” alisema Mathew.

“Dah !. Sikujua kama mambo ni makubwa kiasi hiki”

“Mambo ni makubwa na yanazidi kuwa makubwa kila uchao kwa sabbau mtandao huo ni mkubwa. Jombaa tutazungumza zaidi tukipata

nafasi lakini kwa sasa nimekuja kukujulia hali na kukuomba jambo moja”

“Jambo gani Mathew?

“Mimi na wenzangu leo hatutakuwepo hapa nyumbani. Tutakuwa na misheni Fulani muhimu sana. Naomba uwe mwangalizi wa hapa hadi nitakaporejea. Hakuna mtu wangu yeyote anayefahamu mahali hapa hivyo kabla hatujarudi hakuna anayeruhusiwa kuingia humu ndani”

“Usihofu kuhusu hilo. Ilimradi mniache silaha”

“Silaha utapata.”

“Vipi kuhusu yule mwanamke? Mnaondoka naye?

“Anaitwa Regina. Yeye atabaki hapa kwani naye anatafutwa kama wewe. Ule mzigo wa yale mauaji umemuangukia yeye na kwa sasa anatafutwa na jeshi la polisi.”

“Mathew usihofu, kila kitu kitakuwa salama hapa

nyumbani” alisema Jombaa huku akijiweka sawa.

“Ahsante Jombaa.” Alisema Mathew na kutoka akaenda kugonga mlango wa chumba cha Regina. Aliufungua mlango na kumkaribisha Mathew ndani.

“Mathew nini kinaendelea tangu tulipoachana ile alfajiri? Gavana amepatikana? Aliuliza Regina.

“Hapana. Gavana hajapatikana hadi muda huu. Regina nimekuja kukutaarifu kuwa mimi na wenzangu

hatutakuwepo hapa nyumbani kwa siku ya leo. Tunakwenda katika msiba wa Bernadetha. Tunaamini kuna kitu tutakipata huko. Utabaki hapa nyumbani na Jombaa”

“Mathew ninamuogopa sana yule jamaa. Macho yake yanatisha”

“Huna sababu ya kumuhofia. Hana tatizo lolote” alisema Mathew.

“Mathew ninatamani sana na mimi ningekwenda katika msiba wa huyo mwanamke aliyetuma watu waniue.

Ninatamani ningeipata walau picha yake nimuone alivyo.” Alisema Regina.

“Kitu kikubwa tunachokifanya kwa sasa ni kutafuta kama kuna muunganiko kati ya mtandao wa akina Bernadetha na chama cha ukombozi wa Afrika ambacho unahisi ndio wanaotaka kukuua. Kama Israel Maungwana atahudhuria msibani basi tutakuwa na uhakika mkubwa wanashirikiana. Tutakujulisha pale tutakapopata chochote”

alisema Mathew na kutoka akawafuata akina Gosu Gosu.

Kwa maongozi ya Ruby walimaliza kuweka garini kila kifaa walichokihitaji. Maandalizi yote yalipokuwa tayari Mathew alimfuata Jombaa akampatia bastola. Ruby aliwasiliana na Ambola ambaye tayari alikwisha fika msibani nyumbani kwa mzee Perfect, akawaelekeza mahali msiba ulipo, safari ikaanza.

****

Gavana Jackson Mzumile alihisi joto kali kiasi cha kushindwa kupumua. Mwili wote uliloana jasho kama vile amemwagiwa ndoo nzima ya maji. Alimlilia Mungu amsaidie amuondoe katika mateso yale.

Akiwa katikati ya mateso makubwa, mlango ulifunguliwa jamaa wale watatu wakaingia tena. Kama ilivyokuwa mwanzoni jamaa wawili walijiegemeza ukutani

na kumpa nafasi yule mwenzao kumuhoji.

“Gavana tumerejea tena” alisema yule jamaa baada ya kuketi kitini.

“Vijana wangu ninawaombeni mniondoe katika mateso haya. Siwafahamu wale watu mlioniuliza” alisema Gavana.

Kiyoyozi kiliwashwa na hali ya hewa ikawa ya ubaridi.

“Gavana naamini katika muda huu tayari umefanya tafakari ya kutosha. Uko

tayari kutupa majibu? Aliuliza yule jamaa.

“Jamani naombeni mniamini. Siwafahamu wale watu mlionionesha picha zao. Kama ningewafahamu nisingekubali kuteseka namna hii” alisema Gavana.

“Gavana, wewe mwenyewe ndiye unayejichelewesha kutoka humu ndani. Ninakuhakikishia ukitueleza ukweli tutakurejesha nyumbani. Ukiendelea kutudanganya utaendelea kukaa hapa ndani

kwa muda usiojulikana na yawezekana usitoke tena humu ndani. Hakuna atakayekusaidia Gavana kutoka nje kama unavyodhani. Hakuna anayefahamu kama uko hapa hivyo usitegemee kama msaada utakuja. Hebu jenga picha namna mke wako anavyoteseka hivi sasa baada ya kupata taarifa umetekwa. Usiendelee kumpa mateso hayo mkeo unayempenda. Tueleze ukweli tukurejeshe nyumbani ukaungane na mkeo, ndugu na jamaa.” Alisema yule jamaa.

“Vijana wangu, hao watu siwafahamu. Kama ningewafahamu ningewaambia. Hata mimi sipendi kuteseka kiasi hiki.” Alisema Gavana.

Yule jamaa alivua miwani na kumtazama Gavana. Macho yake mekundu yalitisha.

“Naitwa Red eyes au niite Red inatosha sana. Mimi si mtu mbaya lakini pale ninapolazimishwa kuwa mbaya hata shetani huwa mzuri. Usitake Gavana kunilazimisha niwe mtu

mbaya, kwa sababu hata mimi sipendi kuwa mbaya. Naomba tafadhali unieleze kuhusiana na watu hawa ambao nina uhakika mkubwa unawafahamu” alisema Red.

“Siwafahamu hawa watu jamani naomba mniamini” alisema Gavana.

“Sawa Gavana. Inaonekana unalifurahia joto hili humu ndani. Endelea kuburudika na pale utakapokuwa tayari kuzungumza utabonyeza hiki

kidude” alisema Red na kuweka kidude Fulani mezani.

“Jamani naombeni vijana wangu mnisikilize” alisema Gavana lakini wale jamaa waliondoka kama vile hawana masikio ya kusikia. Mlango ulifungwa ikawaka taa yenye mwangaza mkali na hali ya hewa ikabadilika. Joto lilianza.

“Natakiwa kujitahidi kuvumilia mateso haya. Nikifunguka na kukiri ninamfahamu Mathew Mulumbi, hawa wanaharamu watafanikiwa mipango yao.

Sitaki hilo litokee. Mipango yao haipaswi kufanikiwa katika ardhi ya Tanzania. Kwa hili niko tayari hata kuutoa uhai wangu kuliko kusema ukweli. Ni Mathew Mulumbi pekee ambaye nina uhakika anaweza akafanikiwa kuupata ukweli kuhusu Kelvin. Ndani ya kipindi kifupi tayari amekwisha piga hatua na kufahamu mambo mengi ikiwamo Kelvin kuwa mpelelezi wa siri wa SNSA. Sikulifahamu jambo hili. Mathew Mulumbi ni hazina ambayo inapaswa kulindwa

kwa gharama zozote hata ya uhai wangu” aliwaza Gavana huku joto likizidi kupanda.

“Bado najiuliza hawa jamaa wamewezaje kujua kama nilikutana na Mathew Mulumbi na Faraji usiku wa jana? Makutano yetu yalikuwa ya siri sana lakini wameweza kufahamu. Bado najiuliza walifahamuje kama nitakwenda kanisani asubuhi. Kwa namna tukio lile lilivyotokea inaonesha wazi walikuwa na uhakika mkubwa na kile walichokuwa wanakifanya. Hawakuwa

wanabahatisha. Je wamekuwa wananifuatilia kwa muda mrefu? Ninajiuliza pia kuhusu wale wapelelezi wote niliowaweka kuchunguza kutoweka kwa Kelvin, ni vipi waliweza kufahamika na kuuawa? Gavana aliendelea kujiuliza maswali.

“Kuna mtu mmoja tu anaweza akanisaidia kupata majibu ya mswali haya magumu naye ni Mathew Mulumbi. Natakiwa kuendelea kuvumiklia mateso haya kwa ajili yake”

****

Taarifa za kifo cha Bernadetha zilisambaa kwa kasi ya moto wa nyika. Saa saba mchana tayari nyumbani kwake watu walikuwa wamefurika. Kutokana na uwingi wa magari, sehemu iliyotengwa kwa ajili ya kuegesha magari ilijaa hivyo kulazimisha magari mengine kuelekezwa kwenda kuegesha katika uwanja wa Gofu uliokuwa mita chache kutoka katika nyumba ya jaji mstaafu Perfect Lyimo.

Gari la akina Mathew lilikuwa miongoni mwa magari yaliyoelekezwa kuegesha katika uwanja wa Gofu ambao tayari nusu yake ulikuwa umejaa.

“Eneo hili ni zuri kwa sisi kuifanya kazi yetu” alisema Mathew.

Gari lao lilikuwa na vioo vyeusi pamoja na mapazia kwa ndani. Mtu aliyeko nje hawezi kuona kile kinachofanyika ndani ya gari.

“Ruby kazi ianze mara moja.” Alisema Mathew na

Ruby aliyekuwa katika kiti cha dereva alirudi nyuma na kuanza uchawi wake katika kompyuta. Alifungua dirisha kidogo na kutoa nje drone ambayo wamekuwa wakiitumia sana katika misheni zao mbali mbali ambayo iko katika umbo la ndege ambaye alipaa kuelekea nyumbani kwa Jaji Perfect. Hakuna aliyemtilia mashaka ndege yule ambaye alionekana kama ndege halisi tena wa kuvutia. Kupitia kamera zilizofungwa kwa ndege yule, walianza kupata picha kutokea

juu. Ruby alimtafutia sehemu nzuri ndege yule akatua mahali ambako waliweza kuona kwa urahisi kila kilichokuwa kinaendelea. Kulifungwa mahema kwa ajili ya kuwakinga waombolezaji na jua. Katika hema lililokuwa mbele kabisa ya nyumba kuliwekwa sofa nzuri hizi zilikuwa kwa ajili ya watu maalum. Katika viti vilivyokuwa upande wa pili, akina Mathew waliweza kumuona Ambola ambaye alikuwa amejitanda mavazi meusi. Pembeni yake

alikuwepo Jackline Mo. Naye alikuwa katika mavazi meusi huku ameivaa miwani ile aliyopewa aivae.

Kwa zaidi ya dakika thelathini walikuwa wanajaribu kumuhamisha ndege kutoka sehemu mbali mbali kuwachunguza watu waliokuwepo pale msibani na wale waliokuwa wanaendelea kuwasili.

“Hakuna sura ya Israel Maungwana.” Alisema Ruby.

“Kama ana mahusiano na Bernadetha lazima atakuja.

Tunatakiwa kuwasiliana na Ambola kujua kama amefanikiwa kumuona Israel.” Alisema Mathew na Ruby akampigia simu Ambola.

“Hallow” alisema Ambola kwa sauti ndogo. Aliinuka kutoka mahali pale alipokuwa akasogea mbali kidogo.

“Ambola tayari tumefika na tayari tumekwisha anza kupata picha za hapo msibani.”

“I’m sorry nilisahau kuuvaa ule mkufu ulionipa”

“Usijali. Umefanikiwa kumuona yule mtu tuliyekuonesha picha yake?

“Mpaka sasa sijamuona. Labda atakuja baadaye” alijibu Ambola

“Vizuri. Endelea kufuatilia na kuchunguza. Kama utaona kitu chochote ambacho si cha kawaida tujulishe tafadhali tuko hapa karibu” alisema Ruby na kukata simu.

“Mpaka sasa Israel hajafika” Ruby aliwaambia akina Mathew.

“Tuendelee kusubiri na kuchunguza kila kitu kinachoendelea. Lazima kuna kitu tutakipata” alisema Mathew.

Baada ya saa mbili kupita wakiendelea kufatilia kila mtu aliyekuwa akiingia nyumbani kwa jaji mstaafu Pefect Lyimo, hatimaye watu wapatao nane walijipanga mstari.

“Kuna tukio linakwenda kutokea hapa” alisema Mathew.

Dakika chache baadaye, msafara wa kiongozi mmoja

mkubwa uliwasili msibani pale. Kutoka katika msafara ule alishuka rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania Dr Nehemia Nchelela. Alipokewa na Jaji mstaafu Perfect Lyimo.

“This is much harder that we think” alisema Mathew.

“Mathew una maanisha nini? Aliuliza Ruby.

“Rais pia ni mtu wa karibu na familia hii.” Alijibu Mathew.

“Mathew usiache tukafikiri kama unavyofikiri” alisema

Gosu Gosu akimtazama Mathew kwa sura iliyojaa maswali mengi.

“Gosu Gosu inawezekana kabisa kile nikifikiriacho kikawa kweli”

“Siwaelewi mnamaanisha nini ninyi watu” alisema Ruby.

“Nilivyomuelewa Mathew, wasiwasi wake ni kuwa Rais anaweza akawa katika mtandao wa akina Perfect” alisema Gosu Gosu.

“Hilo pia linawezekana kabisa. Mtandao huu ni

mkubwa na wenye nguvu” alisema Ruby.

“Kuna mambo kadhaa yanayonifanya nihisi kuwa yawezekana mkuu wa nchi pia ni mmoja wa waliomo katika mtandao huu. Idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi SNSA iko chini ya ofisi yake. Faraji Dilele alitolewa katika nafasi yake ya ukurugenzi wa idara hiyo bila sababu na mpaka sasa hajapangiwa kazi nyingine yoyote ya kufanya japo kuna tetesi kuwa anaweza akapewa ubalozi.”

“Unawezaje kutolewa katika nafasi nyeti kama ile bila kuambiwa sababu? Gosu Gosu alihoji.

“Ni kweli lazima tujiulize swali hilo kwa sababu Fraji alitolewa katika nafasi yake bila kuambiwa sababu na hakuruhisiwa kukanyaga tena katika ofisi za SNSA. Kiongozi mkuu wa idara ya SNSA ni rais wa nchi hivyo kuondolewa kwa Faraji ni wazi Rais ndiye aliyemuondoa. Swali linaloibuka kwa nini amuondoe Faraji kwa staili ya namna hii?

“Lazima ipo sababu kubwa.” Alisema Ruby

“Kuna jambo moja alinieleza Faraji ambalo ninalipa uzito. Kelvin Mzumile mtoto wa Gavana ambaye alikuwa ni mpelelezi wa siri wa SNSA, alikuwa anachunguza tetesi za Rais mstaafu Malaki Mnambara kuwa hai. Kama mnavyofahamu Rais mstaafu Mnambara alifariki akiwa nje ya nchi lakini kifo chake kilizua utata hapa nchini na baadaye ziliibuka tetesi za Raisi huyo kuwa hai. Kabla hajatoweka, Kelvin

alimwambia Faraji aliyekuwa mkurugenzi wa SNSA wakati huo kwamba, alikaribia sana kuufikia ukweli kuhusiana na tetesi hizo za Rais mstaafu Mnambara kuwa hai. Kwa bahati mbaya Kelvin alitoweka kabla hajampa Faraji taarifa ya uchunguzi wake. Wiki moja baada ya Kelvin kutoweka, Faraji naye alitolewa katika nafasi yake ya ukurugenzi. Mtaona namna mambo haya yalivyotokea kwa kufuatana. Naamini kupotea kwa Kelvin na Faraji kutolewa katika nafasi ya ukurugenzi wa SNSA,

kuna mahusiano na tetesi za Rais mstaafu Mnambara kuwa hai.” Mathew alinyamaza kidogo na kuyaelekeza macho yake katika kompyuta. Rais alikuwa ameketi sofani akizungumza na wanafamilia akiwepo Ambola.

“Kwa mujibu wa maelezo ya Regina, Rais mstaafu Mnambara anahusishwa na chama cha ukombozi wa Afrika. Regina anasema kuwa Mnambara ana hasira na chama chake baada ya kukataa kumuunga mkono nia yake ya kufanya marekebisho ya katiba

ili aweze kuendelea kutawala. Anataka kukiondoa madarakani chama kinachotawala na kukiweka chama cha ukombozi wa Afrika alichokiasisi kwa siri. Kupotea kwa Kelvin na kuondolewa kazini Faraji ni mipango ya kuhakikisha ukweli wa jambo hili haujulikani. Dr Nehemia amechangia katika suala hili kwa kumtoa Faraji katika nafasi yake ili ukweli usijulikane. Kitendo chake cha kuonekana msibani kwa Bernadetha kinaacha maswali je naye anashirikiana na

mtandao huu?. Mimi kwa upande wangu nimeanza kuhisi lazima atakuwa anahusika lakini uchunguzi wa kina unatakiwa" alisema Mathew.

"Mathew, kwa ufafanuzi huo hata mimi sasa kuna kitu ninanza kukiona. Upo uwezekano mkubwa Rais akawa ni muhusika wa mtandao huu." Alisema Gosu Gosu.

"Tuendelee kuchunguza tutaupata ukweli." Alisema Mathew.

Rais alitumia dakika ishirini pale nyumbani kwa jaji mstaafu Perfect Lyimo. Aliagana na wanafamilia kisha akaondoka.

“Ruby mpigie simu Ambola mkumbushe kuwa tunahitaji kufuatilia mawasiliano ya Perfect hivyo afanye juu chini kuhakikisha ile program iliyowekwa katika simu yake inafanya kazi.” Alielekeza Mathew. Ruby alichukua simu akampigia Ambola akampa yale maelekezo.

****

Mlango wa chumba alimokuwa Gavana ulifunguliwa, Red na watu wake waliingia kwa kasi ndani ya chumba kile. Haraka haraka Gavana alifunguliwa pingu akatolewa nje ya chumba. Alikuwa amepoteza fahamu. Aliingizwa katika chumba kingine chenye hewa ya kutosha akalazwa kitandani kisha akawekewa puani kifaa cha kumsaidia kupumua. Watu wale walifanya mambo haraka haraka, walionekana kufahamu mambo mengi.

Baada ya dakika kadhaa Gavana alizinduka na kujikuta katika kile chumba chenye hewa safi. Machozi yalimtoka baada ya kuwaona wale jamaa wakiwa wamekizuguka kitanda chake.

“Kwa nini mnanitesa namna hii vijana? Nimewakosea nini? Aliuliza Gavana.

“Pole sana mheshimiwa Gavana. Sisi siyo watu wabaya kama nilivyokwambia, lakini haya yote umeyataka wewe mwenyewe. Ninarudia tena

kukuomba tueleze ukweli kuhusu wale watu kama unawafahamu. Ukitueleza ukweli ninakuahidi tutakurejesha nyumbani kwako haraka sana lakini kama ukiendelea kutudanganya na kukana kuwa huwafahamu zoezi hili litaendelea.” Alisema Red.

“Nimekwisha waambia ukweli, watu wale siwafahamu. Ni mara ya kwanza ninaziona picha zao. Naomba mniamini tafadhali” alisema Gavana.

“Gavana tunajua unatudanganya. Watu wale unawafahamu ni washirika wako lakini hutaki kukiri. Haya yote umeyachagua wewe mwenyewe hivyo usitulaumu sisi” alisema Red na ukimya ukapita.

“Gavana ninakuuliza kwa mara nyingine tena wale watu niliokuonesha picha zao unawafahamu? Aliuliza Red.

“Hapana siwafahamu” alijibu Gavana.

Red aliwatazama wenzake akavua miwani yake na kusema.

“Bado anaendelea kuficha siri. Mtoeni humu tafadhali zoezi liendelee.”

“Jamani naomba msinirudishe katika kile chumba. Niueni lakini si kunirejesha katika kile chumba cha joto! Alilia Gavana.

“Sisi si wauaji, hatutakuua lakini tutakutesa hadi pale utakapoamua kutueleza ukweli.” Alisema Red. Gavana alibebwa juu kwa juu na wale

jama wenye nguvu hadi katika chumba kingine.

“Gavana umekataa joto sasa tumekuleta humu ili upunguze joto” alisema Red.

Ndani ya kile chumba alimoingizwa Gavana, kulikuwa na tanki la maji lenye ujazo wa lita elfu moja. Lilikuwa ni tanki la chuma. Gavana alivuliwa nguo akafugwa mikono na miguu halafu akaingizwa ndani ya yale maji. Mdomoni alibandikwa gundi ili asiweze kusema chochote.

Yalikuwa ni maji meupe ya baridi sana. Baada ya sekunde chache tangu aingizwe k atika maji yale, Gavana alianza kuhisi kama sindano ndogo ndogo zinauchoma mwili wake ndipo alipogundua yale yalikuwa ni maji yaliyowekwa dawa ya kuwasha. Red aliyaelekeza macho yake katika saa yake ya mkononi.

Mwili wa Gavana ulianza kuwasha. Alitamani apige kelele ili atolewe katika yale maji lakini hakuweza alikuwa amebandikwa gundi mdomoni. Yalikuwa ni mateso makali.

Muwasho ulizidi, alishindwa kujikuna kwani mikono ilikuwa imefungwa. Alibaki akiporomosha machozi akimlilia Mungu. Mateso yalikuwa makali sana.

Baada ya dakika kumi, alitolewa katika yale maji. Tayari mwili ulikuwa umevimba. Ile gundi mdomoni ilibanduliwa. Gavanba alikuwa anahema haraka haraka.

“Gavana uko tayari kusema ukweli? Aliuliza Red. Gavana alikuwa anaweweseka

kwa muwasho mkali katika mwili wake.

“Mpelekeni akapumzike kwanza” alielekeza Red na Gavana akapelekwa katika chumba kingine akasukumiwa ndani. Alihisi mwili unawake moto.

Baada ya saa moja ya mateso makali, mlango wa kile chumba ulifunguliwa wakaingia tena akina Red. Jamaa mmoja alimpulizia Gavana dawa fulani mwilini ambayo ilimfanya asihisi tena ule muwasho.

“Pole sana Gavana” alisema Red huku akitabasamu.

Gavana alimtazama lakini alishindwa kuongea akaangusha machozi.

“Gavana tumekuja tena na unafahamu kitu gani kilichotuleta hapa. Tunataka ukweli. Kama hautaeleza ukweli mambo yatakuwa magumu sana kwako kwani kadiri unavyokuwa mbishi kuzungumza chochote ndivyo unavyotulazimjisha tuongeze kiwango cha mateso. Tusipote

muda, uko tayari kuzungumza ukweli? Aliuliza Red.

“Si. . si. . siwafahamu wale watu.” alisema Gavana huku akitetemeka.

“Gavana naomba utueleze ukweli mzee wangu ili tuachane na hili zoezi. Hatupendi kukutesa mtu muhimu kwa nchi kama wewe lakini tunahitaji utueleze ukweli” alisema Red.

“Nimekwisha waambia siwafahamu hawa watu. Niko tayari hata mniue lakini huo ndio ukweli” alisema Gavana.

Red alivua miwani akawatazama wenzake kisha akatoa maelekezo. Gavana alitolewa ndani ya kile chumba akapelekwa katika chumba kingine kilichokuwa na meza na viti viwili. Aliwekwa katika kiti halafu kikaletwa chakula akawekewa mezani akaachwa ale.

Red alichukua simu akampigia mkuu wake.

“Red nipe habari. Kuna mfanikio yoyote hadi sasa?

“Boss mpaka sasa bado huyu mzee hajafunguka

chochote. Bado amesimamia msimamo wake wa kutowafahamu wale watu.”

“Anaonekana ni mtu mwenye msimamo mkali sana. Hakuna kuchoka zoezi liendelee hadi atakaposema ukweli”

“Boss kuna kitu nimekiona kutoka kwa huyu mzee”

“Umeona nini Red?

“Huyu mzee hawezi akafunguka kirahisi na mpaka sasa yuko tayari hata kuutoa uhai wake kuliko kusema

ukweli. Tunatakiwa tuongeze nguvu. Tukiendelea na mateso haya madogo madogo tutapoteza muda mwingi na huyu mzee hatafunguka. Tunaomba ruhusa yako boss ili tutumie njia nyingine" alisema Red. Kilipita kimya kifupi.

"Nini ushauri wako Red? Lazima Gavana afunguke kwani tunahitaji sana kuwafahamu mahali walipo wale watu"

"*Boss*, mimi ushauri wangu tumtumie mke wake. Kama tukitishia kumuua mke

wake nina uhakika mkubwa lazima atakubali kusema ukweli. Kwa watu wagumu kufunguka kama huyu mzee, njia pekee ya kuwafungua ni kutishia kuteketeza familia zao” alisema Red ukapita tena ukimya mfupi.

“Sawa Red. Ni wazo zuri pia.Niachie nilifanyie kazi, nitakupa jibu baada ya muda mfupi.”

Simu ilikatwa, Red akarejea katika chumba cha mapumziko, akamimina mvinyo katika glasi

akagugumia wote na kuwasha sigara.

****

Mlango ulifuguliwa tena, Red na wenzake wakaingia chumbani. Sahani zilikuwa tupu. Gavana alimaliza chakula chote alichopewa.

“Hello Gavana. Tumerejea tena. Safari hii nataka tuzungumze kirafiki.” Alisema Red.

“Kwa nini mnanitesa namna hii vijana? Kwa nini mnanidhalilisha kiasi hiki? Nimewakosea nini? Aliuliza Gavana.

“Gavana ulichotukosea ni kuficha ukweli kuhusu wale watu niliokuonesha picha zao. Tunachohitaji tueleze mahali walipo ili tukurejeshe nyumbani kwako. Gavana narudia tena kukuhakikishia kuwa ukitueleza ukweli, tutakurejesha nyumbani kwako haraka sana”

“Kwani ninyi ni akina nani?

“Gavana uko hapa kujibu maswali na si kuliza maswali. Ninaomba utuokolee muda na utueleze ukweli tafadhali”

“Jamani hao watu ambao mnanilazimisha niwaeleze ukweli, siwajui. Ni mara ya kwanza ninaziona picha zao. Naomba mniamini tafadhali” alisema Gavana.

“Gavana, huna sababu ya kuendelea kutuficha kwa sababu tayari tunaufahamu ukweli.” Alisema Red na

kuitafuta video Fulani katika kishkwambi chake akaicheza na kumuonesha Gavana.

“Hebu tazama mwenyewe. Nitarudi baada ya muda mfupi” alisema Red na kuinuka akatoka nje akamuacha Gavana akitazama video ile.

Katika video alionekana mwanamke akiwa amefungwa kwenye kiti, kichwani akiwa amefunikwa mfuko mweusi. Baada ya sekunde chache jamaa mmoja ambaye naye alikuwa amefunika uso wake

na kuacha macho pekee alimsogelea mwanamke yule akamtoa mfuko kichwani. Gavana alipatwa na mshituko mkubwa.

“Lucy ! alisema Gavana. Mwanamke aliyeonekana katika video ile ni mke wake. Mwili ulimtetemeka kwa hofu.

“Hawa mashetani wamefika hadi kwa mke wangu! aliwaza akiendelea kuitazama video ile.

Jamaa yule aliyeufunika uso wake kwa kofia iliyoacha

sehemu ya uso pekee, alijitokeza akavuta kiti akaketi.

“Hallo Lucy” alisema yule jamaa na kumshangaza Gavana.

“Hawa jamaa wanalifahamu hadi jina la mke wangu. Hawa ni watu hatari sana” aliwaza Gavana.

“Mnataka nini kwangu? Aliuliza Lucy ambaye nywele zake zilitimuliwa na uso wake ulikuwa na damu. Ilionekana alikuwa ameteswa kabla ya video ile kuanza kurekodiwa.

“Lucy sisi ndio tunaomshikilia mume wako.” Alisema yule jamaa.

“Mume wangu amekosa nini hadi mkamteka?

“Hajatukosea chochote, kuna mambo muhimu tunayahitaji kutoka kwake ndiyo maana tukamchukua lakini amekuwa mgumu kutoa ushirikiano ndiyo maana tumekufuata wewe. Hii ni nafasi yako ya kumuokoa mume wako. Kama utashindwa kutoa ushirikiano basi hutamuona tena mume

wako akiwa hai. Utamuona akiwa ni mfu” alisema yule jamaa.

“Jamani naombeni msimuue mume wangu. Ndiye kila kitu kwangu. Nitawapa kiasi chochote cha fedha mnachokihitaji ili kumuokoa. Semeni niwape kiasi gani cha fedha ili mumuache huru? Alilia Lucy .

“Mama, sisi hatuhitaji fedha. Kuna mambo ambayo tunahitaji atueleze na akitueleza hayo sisi tutamrejesha hapa nyumbani

mara moja. Hatutaki kumuumiza mumeo wala kumuua lakini ameendelea kuwa kiburi ndiyo maana tumekuja kwako ili kuzungumza nawe umuokoe mumeo.”

“Jamani niko tayari kwa lolote lile kwa ajili ya kumuokoa mume wangu. Kitu gani mnakihitaji? Aliuliza Lucy. Yule jamaa alitoa simu yake akafungua sehemu ya kuhifadhia picha, akaitafuta picha na kumuonesha Lucy.

“Unamfahamu huyu mtu? Umewahi kumuona mahali? Aliuliza yule jamaa. Lucy aliitazama kwa makini sana ile picha. Gavana alitetemeka.

“Lucy please don’t say anything ! alisema Gavana kama vile yuko pamoja na Lucy. Alikuwa amechanganyikiwa.

“Huyu mtu nimemuona hapa nyumbani jana. Ni mara ya kwanza kumuona.” Alisema Lucy

“*Lucy no ! don’t say anything !* alifoka Gavana.

“Unaweza ukatueleza anaitwa nani? Aliuliza yule jamaa.

“Alipokuja hapa alikuwa na mazungumzo ya faragha na mume wangu. Alipoondoka nilimuuliza mume wangu yule mtu ni nani akaniambia anaitwa Mathew Mulumbi”

“Una hakika hujawahi kumuona kabla ya jana?

“Hapana sijawahi kumuona nyumbani kwetu kabla ya jana”

“Vizuri sana. Unaweza ukatueleza nini hasa kilichomleta Mathew nyumbani kwenu?

“Sifahamu. Mazungumzo yao yalikuwa ya faragha na mimi sikuhusishwa” alijibu Lucy.

“Lucy kumbuka hapa unapigania uhai wa mume wako mpenzi hivyo nakusisitiza tueleze ukweli. Ukituficha kitu chochote mume wako atauawa”

“Jamani naombeni msimuue mume wangu,

nitawaeleza ukweli. Kilichomleta Mathew Mulumbi kwa mume wangu ni kuhusiana na kifo cha mtu ambaye mume wangu alimuweka apeleleze tukio la kutoweka kwa mwanetu Kelvin.”

“Vizuri sana.” Alisema yule jamaa na kufungua picha nyingine akamauonesha Lucy.

“Huyu unamfahamu?

“Ndiyo ninamfahamu. Anaitwa Faraji Dilele. Ni rafiki wa mume wangu.”

“Lini ameonekana nyumbani kwenu?

“Jana usiku. Alikuja jana akafanya mazungumzo na Gavana pamoja na Mathew Mulumbi.”

“Ni hayo ambayo tuliyahitaji kutoka kwa mume wako lakini ameshindwa kutoa ushirikiano na kuyaweka maisha yake hatarini. Kuna kitu kimoja cha mwisho ambacho tunataka utuambie. Mathew Mulumbi anaishi wapi?

“Sifahamu. Ni Gavana pekee anayefahamu”

“Lucy tafadhali, tueleze ukweli”

‘Nawaambia ukweli. Sifahamu Mathew anakoishi” alijibu Lucy.

“Sawa. Ahsante hata hivyo kwa kutoa ushirikiano.” Alisema yule jamaa na video ikafika mwisho. Gavana aliweka mikono kichwani. Alichanganyikiwa.

“Kwa nini Lucy amesema ukweli? Ameharibu kila kitu.

Wanawake si watu wa kushirikisha siri yoyote.” Aliwaza.

“Nimevumilia mateso, sikusema chochote lakini washenzi hawa wamezunguka na kumfuata mke wangu wakamtishia akatoa siri. Kila kitu nilichokifanya kimepotea bure. Kuvumilia kote mateso kumbe nimefanya kazi bure. Imeniumiza mno. ! aliendelea kuwaza Gavana.

Alirudia tena kuitazama video ile. Alishindwa kuyazuia machozi kumtoka.

Akiwa katika hali ya kukata tamaa mlango ulifunguliwa akina Red wakaingia.

“Pole Gavana, lakini imetulazimu kufanya kila tuwezalo kuufahamu ukweli. Huna haja ya kuendelea kutuficha tena kwani kama ulivyoona mke wako ametueleza kila kitu tayari. Kuna kitu kimoja tu ambacho tunakihitaji kutoka kwako kabla ya kukurejesha nyumbani kwako. Tunataka utuambie Mathew Mulumbi yuko wapi? Aliuliza Red.

Gavana aliwataza wale jamaa waliokuwa wamesimama mlangoni akamtazama na Red halafu akaangua kicheko.

“Kitu gani kinakufurahisha Gavana? Aliuliza Red.

“Nimewatazama majitu ya miraba minne nikashangaa kwa nini mmeshindwa kupata mnachokihitaji kutoka kwa mwanaume mwenzenu hadi mkamfuata mwanamke. Nimewashangaa sana. Ninyi wanaume wa namna gani?

alihoji Gavana na kusindikiza na kicheko kidogo.

“Gavana hatuhitaji mzaha tunachohitaji ni kujua mahali alipo Mathew Mulumbi. Tuokolee muda tuoneshe alipo tukuache uende zako tafadhali” alisema Red na kumtazama Gavana.

“Neno langu la mwisho kwenu ni hili. Niko tayari kufa lakini si kuwaonesha mahali aliko Mathew Mulumbi. Yule ndiye mwanaume tofauti na nin…. .” Kabla hajamalizia sentensi yake Gavana alijikuta

akiwa sakafuni huku damu ikimtoka mdomoni. Alikuwa ametandikwa kofi zito kutoka katika mkono wenye nguvu wa Red. Aliinuliwa akaketishwa kitini.

“Japokuwa wewe ni mzee wetu lakini naomba uwe na adabu. Sasa muda wa mzaha umekwisha. Utatueleza mahali alipo Mathew Mulumbi? Aliuliza Red. Alivua kiwani na sura yake ilitisha mara mbili.

“I’m ready to die.” Alisema Gavana na kufumba macho.

“Gavana fumbua macho yako. Hatutakuua wewe ila badala yako atakufa mkeo Lucy.”

Gavana alipatwa na mshituko akafumbua macho.

“No ! Please don’t kill her. Hana kosa lolote. Niueni mimi ambaye nimekataa kuwapeni taarifa mnayoihitaji” alisema Gavana.

“Wewe hautakufa kwa risasi utabaki hai. Utakufa kwa mateso ya kumuwaza mke wako” alisema Red.

“Naombeni vijana msimuue mke wangu. Hajawakosea chochote” aliomba Gavana.

“Gavana una njia moja tu ya kumuokoa mke wako nayo ni kutuonesha alipo Mathew Mulumbi. Uko tayari? Aliuliza Red. Gavana alishindwa kujibu alibaki anatetemeka.

“Hauko tayari kumuokoa hata mke wako. Twende ukashuhudie uhai unavyomtoka mke wako” alisema Red na kuwapa maelekezo wale jamaa

maelekezo ya kumtoa Gavana ndani ya kile chumba.

Gavana aliingizwa ndani ya chumba kingine kilichokuwa na runinga kubwa akaketishwa kitini.

“Gavana kabla ya kuwasha runinga hii ili ushuhudie namna uhai unavyomtoka mke wako, nataka nikuulize kwa mara ya mwisho. Je uko tayari mke wako auawe au utatueleza mahali alipo Mathew Mulumbi? Aliuliza Red.

“Kwanini mnataka kutoa uhai wa kiumbe wa Mungu

asiye na hatia yoyote? Aliuliza Gavana.

Red hakumjibu kitu, alielekeza runinga iwashwe. Runingani alionekana mke wa Gavana akiwa amepigishwa magoti. Pembeni yake alisimama jamaa mmoja akiwa na bastola akisubiri kupewa maelekezo.

“Gavana nafasi ya mwisho ya kumuokoa mke wako. Where is Mathew Mulumbi? Aliuliza Red. Gavana midomo ilimtetemeka. Alishindwa kuongea.

“Gavana mbona umegeuka bubu ghafla? Unayemuona runingani ni mke wako na kama hutatueleza mahali alipo Mathew Mulumbi ndani ya sekunde kumi kuanzia sasa mkeo atauawa. Yawezekana unahisi huu ni mchezo wa kuigiza. Ngoja nikuoneshe kuwa hiki ni kitu cha kweli kabisa.” Alisema Red na kuchukua simu yake akaitafuta namba Fulani akapiga. Katika runinga alionekana yule jamaa aliyekuwa amesimama na bastola pembeni ya mke wa gavana akiingiza mkono

mfukoni na kuchukua simu akaipokea na kuweka sikioni.

“Chris, ndani ya sekunde kumi na tano kutoka sasa utaingiza risasi mbili katika kichwa cha huyo mwanamke”

‘Sawa boss.” alisema yule jamaa.

“Gavana muda umeanza kuhesabiwa sasa. Ndani ya sekunde kumi na tano kama hutaeleza mahali alipo Mathew Mulumbi mke wako atauawa” alisema Red na kuitazana saa yake.

“Zimebaki sekunde kumi”

“Jamani msimuue mke wangu. Hana kosa lolote” alisema Gavana. Red hakumtazama. Macho yake aliyaelekeza katika saa yake ya mkononi.

“Sekunde nane zimebaki” alisema Red akiendelea kuitazama saa yake.

“Tafadhali naomba msimuue mke wangu” alisema Gavana. Machozi yalimtoka.

“Five seconds”

“Nawaomba jamani !

“Three seconds !

“Huu mbona mtihani mkubwa sana ! aliwaza Gavana

“One second left ! alisema Red na kumtazama Gavana.

“Gavana muda umekwisha.” Alisema Red na kuinua simu yake akampigia yule jamaa aliyekuwa na Lucy, akapokea. ,

“Kill her ! alisema Red.

“Wait ! Please wait ! alisema Gavana.

“Chris subiri kwanza.” Alisema Red na kumgeukia Gavana.

“Uko tayari kusema? Aliuliza Red.

“Nitawaeleza, tafadhali naomba msimuue mke wangu.”

“Good. Hatutamuua. Tueleze ukweli.”

“Nitawaeleza kila kitu lakini kwanza mfungueni mke wangu awe huru” alisema Gavana. Red alitoa maelekezo mke wa Gavana akafunguliwa

huku Gavana akishuhudia kupitia runinga.

“Tayari mkeo yuko huru. Tueleze ukweli wote kuhusu Mathew Mulumbi na mahali alipo” alisema Red. Gavana alifuta machozi akavuta pumzi ndefu na kusema.

“Sikumfahamu Mathew Mulumbi. Ni yeye aliyenifuata akanijulisha kuhusu kuuawa kwa mpelelezi niliyemuweka kutafuta ukweli kuhusu kupotea kwa mwanangu” alisema Gavana na Red akamkatisha.

“Gavana mke wako amekwisha tueleza kila kitu. Tunachokihitaji kwa sasa ni kujua mahali alipo Mathew Mulumbi” alisema Red.

“Mathew Mulumbi sifahamu mahali alipo kwa sasa” alisema Gavana na Red akavua miwani yake. Sura yake ilionesha hasira.

“Gavana huu si muda wa utani ! alifoka Red.

“Naombeni mnisikilize jamani. Ni kweli sifahamu mahali aliko Mathew Mulumbi. Nilimuuliza mahali

anakoishi lakini aligoma kwa kunieleza ila alichoniambia ni kwamba kwa sasa anatafutwa hivyo yuko mafichoni.”

“Ni namna gani mnawasiliana?

“Hakunipa namba yake ya simu bali ni yeye anayenipigia kila anapohitaji kuonana nami.”

Red alivuruga nywele zake ambazo hakuwa amezichana.

“Gavana naomba utueleze ukweli tafadhali”

“Ninawaeleza ukweli.”

“Gavana ninakupa nafasi ya mwisho kabisa ya kutafakari na kutueleza ukweli. Kama ukishindwa ninakuhakikishia hatutakuwa na huruma tena. Tutamuua mke wako”

“Naomba msimuue mke wangu. Ninawaambia ukweli sifahamu mahali alipo Mathew Mulumbi” alisema Gavana.

“Zoezi litaendelea baada ya dakika kumi. Wakati huo hatutakuwa na huruma kama utashindwa kutuonesha mahali alipo Mathew

Mulumbi” alisema Red na Gavana akarejeshwa katika chumba cha awali. Red alimpigia simu mkuu wake.

“Red, mmepata chochote?

“Boss, huyu mzee yuko tayari kusema lakini bado anasita. Nimempa mapumziko ya dakika kumi kisha zoezi litarudia tena” alisema Red.

“Good. Ni hatua nzuri kama amekubali kueleza ukweli. Nataka muhakikishe safari hii anaeleza kila kitu.Nahitaji jibu kabla ya saa moja jioni.”

“Sawa boss. Nitakupigia baada ya zoezi kukamilika” alisema Red na simu ikakatwa.

Dakika kumi zilimalizika, Red akamfuata Gavana kama alivyomuahidi.

“Gavana muda wa mapumziko umekwisha. Ninataka jibu. Where is Mathew Mulumbi?” aliuliza Red.

“Kwa kweli sifahamu mahali alipo lakini ninaweza kuwasaidia kumpata. Naombeni mnipe dakika chache nitafakari namna ya

kufanya kumpata Mathew Mulumbi”

“Ninakupa dakika tano. Ninaomba uzitumie vyema.” Alisema Red na kutoka.

****

Kiza tayari kilitanda angani akina Mathew waliporejea katika maskani yao.

Baada ya kushuka walielekea ofisini kwao kwa ajili ya kufanya tathmini ya kazi waliyoifanya siku ile. Wakati Ruby akiweka sawa mambo, mlango uligongwa akaingia Regina.

“Poleni kwa kazi ya siku ya leo” alisema Regina.

“Ahsante sana. Natumai mlikuwa na siku nzuri hapa.” Alisema Mathew.

“Hakuna tatizo lolote. Nimekuja kuwapeni pole na kuwajulisha kuwa tayari nimeandaa chakula” alisema Regina.

“Umefanya jambo la muhimu sana. Ninahisi njaa kali” alisema Gosu Gosu.

“Me too” alisema Ruby.

“Sawa tupate kwanza chakula kisha tuendelee na kazi.” Alisema Mathew kisha

wote wakaelekea chumba cha chakula.

“Kuna mafanikio yoyote huko mlikoenda leo? Aliuliza Regina wakiwa mezani wakipata chakula.

“Mafanikio si kama tulivyotegema. Kikubwa tulichokihitaji ni kumuona Israel Maungwana pale msibani lakini hakuonekana. Tutarudi tena kesho na kila siku hadi siku atakapozikwa Bernadetha. Tunataka kujiridhisha kama hawa watu wana mahusiano. Kama wana

mahusiano lazima Israel atahudhuria katika msiba wa Bernadetha lakini kama hatahudhuria ninahisi tutakuwa tunashughulika na makundi mawili” alisema Mathew.

“Leo ni siku ya kwanza. Yawezekana kesho akafika msibani hapo. Kuna kingine chochote mmekigundua? Regina aliuliza.

“Mambo mengi yametokea hapo msibani tumeyarekodi tutayapitia taratibu yawezekana tukapata kitu.”

alisema Mathew. Wakati wakiendelea kula chakula, simu ya Ruby ambayo huitumia kuwasiliana na Ambola iliita akaipokea.

“Hallow Ambola” alisema Ruby.

“Ruby nimefanya kama ulivyonielekeza kuhusu ile pogramu uliyoiweka katika simu yangu. Muda mfupi uliopita nilikuwa na mazungumzo na Perfect na kabla sijakutana naye niliiwasha ile program.

Ninaamini kila kitu kimekwenda vizuri”

“Ahsante sana Ambola. Ninakwenda kufuatilia katika komputa sasa hivi. Kuna kingine chochote ambacho umekipata kwa siku nzima ya leo?

“Yule jamaa ambaye mlinitaka nimchunguze kama atakuja msibani sijamuona” alisema Ambola.

“Sisi pia tulikuwepo hapo kufuatilia kwa karibu lakini hatukumuona.”

“Walikuja wageni wengi akiwemo Rais. Mimi nilijielekeza katika kuchunguza kama yule mtu atakuja msibani”

“Ambola pumzika kwa sasa na kama kuna kitu chochote tutakihitaji kwako tutakujulisha mara moja” alisema Ruby na kukata simu.

“Guys kumekucha. Muda wa kazi” alisema Ruby na kuinuka akakimbia kuelekea ofisini kwao, Mathew na Gosu Gosu nao wakainuka

wakawaacha Regina na Jombaa mezani.

“Ruby kuna nini? Aliuliza Mathew

“Ambola ameifanya ile kazi. Tayari program imeinasa simu ya Perfect Lyimo”

“Good” alisema Gosu Gosu.

Ruby alibonyeza haraka haraka kompyuta yake na kutabasamu.

“Sasa tunaweza kufuatilia mawasiliano yote ya Perfect

anayoyafanya kwa kutumia simu yake” alisema Ruby.

“Kuna chochote mmekipata? Aliuliza Regina aliyeingia mle ofisini.

“Ndiyo. Tumefanikiwa kuipata simu ya Perfect na hivi sasa tunafuatilia mawasiliano yake yote” alijibu Mathew.

“Ni hatua nzuri. Mimi ninakwenda kupumzika . Kama kuna chochote mnakihitaji mtanijulisha” alisema Regina na kutoka kuelekea chumbani kwake.

Wakati wakiendelea na majadiliano mara kulitokea sauti Fulani katika kompyuta ya Ruby.

“Oh my God ! alisema Ruby.

“Kuna nini Ruby? Mathew aliuliza.

“Simu ya Perfect imezimwa” alijibu Ruby.

“Mpigie Ambola tujue kuna tatizo gani” alisema Mathew. Ruby alichukua simu akampigia Ambola.

“Ruby ile program ilifanikiwa kuinasa simu ya Perfect? Aliuliza Ambola.

“Ndiyo Ambola ilifanikiwa lakini kuna tatizo limetokea. Simu ya Perfect imezima ghafla. Unaweza ukajua kwa nini simu hiyo imezima ghafla? Aliuliza Ruby.

“Kwa sasa Perfect hayupo. Aliniambia kuna sehemu anakwenda usiku huu. Atakaporejea nitajaribu kujua nini hasa kilichotokea.” Alijibu Ambola.

“Unadhani amekwenda wapi?

‘Hakusema anakwenda wapi. Atakaporejea nitajua tatizo ni nini hadi simu yake ikazima au yawezekana imeisha chaji kwani siku nzima ya leo alikuwa katika heka heka kubwa”

“Sawa Ambola. Atakaporejea utatujuza”

Ruby alikata simu na kuwageukia akina Mathew akawapa majibu ya Ambola.

“Ruby can you turn on the mic of his phone? Tunahitaji sana kujua kila kinachoendelea. Nina uhakika mkubwa kuna mambo tutayafahamu kama tukifuatilia mazungumzo yake” alisema Mathew.

“Yes I can” alijibu Ruby na kuanza kuinyanyasa kompyuta atakavyo. Baada ya muda akaguna. ,

“Kuna nini Ruby? Mathew aliuliza.

“Betri imeondolewa katika simu hivyo siwezi kufanya chochote” alijibu Ruby.

“Hii inashangaza. Kwa nini ametoa betri? aliuliza Gosu gosu. Ukimya mfupi ulipita kila mmoja akitafakari halafu Mathew akasema.

“Guys kuna kitu yawezekana hakipo sawa. Kitendo cha Perfect kuzima simu na kutoa betri kinashangaza. Kwa nini afanye hivyo baada ya sisi kuanza kumfuatilia? Je aligundua kama simu yake inafuatiliwa?

Kama ndiyo, amefahamuje? Aliuliza Mathew.

“Hili suala linaanza kuwa gumu” alisema Gosu Gosu akiwa ameshika kiuno.

“Guys tusiamimi moja kwa moja kwamba Perfect ameitoa betri katika simu yake. Kuna uwezekano labda chaji imeisha kama alivyosema Ambola. Mambo yalikuwa mengi leo yawezekana alikosa muda wa kuchaji simu yake na ghafla ikamzimikia” alisema Ruby.

“I think I need fresh air” alisema Mathew na kutoka nje.

“Wazo kwamba simu ya Perfect imeisha chaji silikubali. Haiwezekani asijue kama simu yake inakaribia kuisha chaji hasa kwa siku kama ya leo ambayo ni msiba wa mke wake. Anafahamu fika lazima afanye mawasiliano na watu mbali mbali. Ambola anadai kwamba kuna sehemu ameenda ninaanimi hata kama simu yake haikuwa na chaji ya kutosha angeichaji katika gari lake.....”

“Mathew” sauti kutoka katika pembe yenye mwangaza hafifu, ilimshitua Mathew.

Tayari mkono wa Mathew ulikwisha ishika bastola.

“Ni mimi Jombaa” Ilimlazimu Jombaa kujitambulisha haraka baada ya mkono wa Mathew kuichomoa bastla kwa kasi ya kushangaza.

“Jombaa mbona unajificha katika giza?

“Ninapunga upepo” alijibu Jombaa na kuinuka akamfuata Mathew.

“Mathew nilikuwa natafuta nafasi ambayo uko

peke yako nizungumze nawe jambo la muhimu. Kwanza bastola yako hii hapa” alisema Jombaa na kumkabishi Mathew bastola yake. Walikwenda kuketi katika gogo la kupumzikia bustanini.

“Kitu gani unataka kuniambia Jombaa? Mathew aliuliza.

“Mathew wewe ni mtu ambaye kwa sasa ninakuchukulia kama ndugu yangu licha ya kunipiga risasi . Ni wewe ambaye umenifanya nitafakari upya kuhusu maisha

yangu. Tutayazungumza hayo siku nyingine lakini leo asubuhi ulinieleza japo kwa kifupi kile ambacho wewe na wenzako mnakifanya. Ni kitu kikubwa kwa taifa letu. Mimi japo nimekuwa katika ujambazi lakini sijawahi kudiriki kutaka kufanya mambo kama wanayofanya hawa watu kutaka kuuza nchi kwa mabeberu.”Jombaa alinyamaza kidogo. Mathew aliendelea kumtazama kwa shauku ya kutaka kujua kile anachotaka kumwambia.

“Mlipoondoka, ulinipa jukumu la kulinda hapa nyumbani. Hakukuwa na tatizo lolote isipokuwa kuna kitu kuhusu yule mwanamke” Jombaa alinyamaza kidogo halafu akaendelea.

“Nilimsikia yule mwanamke akizungumza na mtu simuni”

“Subiri kidogo Jombaa.Mwanamke yupi unamzungumzia? Regina?

“Ndiyo”

“Alikuwa anazungumza na simu? Mathew alishangaa.

‘Ndiyo. Nilimsikia akizungumza na simu.”

“Una uhakika Jombaa? Aliuliza Mathew.

“Ndiyo Mathew siwezi kukudanganya. Nilikuwa nimetoka nje nimepumzika.Nilimuona akinichungulia dirishani halafu akarejea ndani.Nilihisi kuna kitu hakiko sawa nikarejea ndani taratibu nikaenda katika mlango wake nikamsikia akizungumza na

mtu simuni. Nilijibanza kimya nikasikia mazungumzo yake bila yeye kujua kama nilikuwa mlangoni" alisema Jombaa na kumtazama Mathew.

"Alizunguma nini na huyo mtu?" aliuliza Mathew.

"Nilimsikia akimpa angalizo mtu aliyekuwa anazungumza naye kwamba amwambie mtu Fulani ambaye jina lake sikulisikia vyema asiende msibani. Yule mtu aliyekuwa anazungumza naye inaonekana alitaka kufahamu kwa nini huyo mtu aliyemsema

Regina asiende msibani ndipo alipomwambia kuwa asiende sababu jamaa wameondoka wanakwenda msibani kufuatilia kama atahudhuria. Nilipata wasi wasi kidogo kwa maneno yale kwa sababu uliniambia na ninyi mnakwenda msibani kufuatilia mambo Fulani nikapata hofu huyu mwanamke asije kuwa anawazunguka katika mipango yenu" alisema Jombaa.

Mathew alihisi jasho linamtoka.

“Jombaa naomba unitazame machoni unihakikishie kwamba hiki unachonieleza ni kitu cha kweli” alisema Mathew.

“Mathew sina sababu ya kukudanganya. Wewe ni mtu mzuri sana ambaye umejitolea kunisaidia na kuisaidia nchi. Bila wewe sijui hivi sasa ningekuwa wapi. NInakuheshimu sana siwezi kukudanganya” alisema Jombaa.

“Jombaa hiki ulichoniambia ni kitu kikubwa

sana. Sikujua kama Regina ana simu na kuna watu anawasiliana nao. Una hakika hakugundua kama unasikia mazungumzo yake? Aliuliza Mathew.

“Nina uhakika mkubwa hakunisikia. Alizungumza kwa uhuru mkubwa akijua niko nje.” alisema Jombaa.

Mathew alivuta pumzi ndefu na kusema

“Jombaa kuna kitu nataka tukifanye sasa hivi. Nitakwenda kumchukua Regina chumbani kwake

nitakuja naye hapa nje. Baada ya Regina kutoka utakwenda chumbani kwake utapekua kuitafuta simu. Ukiipata utaificha halafu utatoka nje utatufuata tulipo. Hiyo itakuwa ni ishara kuwa umeipata simu. Kama ukiikosa, toka nje kisha pitiliza kwenda katika mti ule kule, nitakuwa nimepata jibu nitajua nifanye nini" alisema Mathew.

"Sawa Mathew." Alijibu Jombaa na kuinuka kuelekea ndani. Mathew naye aliekekea chumbani kwa Regina

akagonga mlango. Regina aliufungua mlango akakutana na Mathew.

“Mathew” alisema Regina

“Regina tunaweza kuzungumza?

“Sawa, karibu ndani” alisema Regina.

“Nadhani twende tukazungumzie nje” alisema Mathew akiwa amesimama mlangoni. Regina alitoka wakaeleke bustanini wakaketi juu ya gogo.

“Siku yako leo imekwendaje? Aliuliza Mathew.

“Ninashukuru siku imekwenda vyema”

“Are you comfotable here? Aliuliza Mathew na Regina akatabasamu.

“Mathew japokuwa nipo kati kati ya matatizo makubwa lakini mahali hapa ninahisi niko salama sana. Ninahisi amani na salama nikiwa nanyi. Ninapata kila kitu ninachokihitaji” alijibu Regina.

“Nashukuru kama unajihisi amani na salama ukiwa hapa. Ninakuahidi kufanya kila lililo ndani ya uwezo wangu kuhakikisha unarudi tena kuishi maisha yako ya kawaida. Suala hili litamalizika japo sina uhakika lini. Vikwazo ni vingi. Hawa watu tunaowachunguza nao pia wamejipanga vyema kuhakikisha mipango yao inakwenda vyema. Leo tulitaka kuchunguza kama Israel na akina Bernadetha ni mtandao mmoja lakini hakuonekana msibani. Hatujakata tamaa,

tutaendelea kuchunguza hadi tuufahamu ukweli” Alisema Mathew. Regina alimeza mate na kusema.

“Ninaelewa Mathew na ninawashukuru sana kwa jitihada ambazo mnaendelea kuzifanya kuhakikisha jambo hili linamalizika.” Alisema Regina na mara Jombaa alitoka ndani akaelekea mahali walipo.

“Huyu jamaa tayari mmeanza kuzungumza? Aliuliza Mathew.

“Nadhani mimi naye damu zetu haziendani. Sina hata mpango wa kuzungumza naye.”

“Nadhani anakuja kujiunga nasi. Kama hujisikii vyema kuwa karibu yake nenda chumbani kwako ukapumzike halafu nitazungumza nawe zaidi baadaye” alisema Mathew.

“Ahsante Mathew.” Ambola aliinuka na kupishana na Jombaa akaelekea chumbani kwake.

“Nipe habari Jombaa” alisema Mathew.

“Simu hii hapa nimeikuta chini ya mto wake.” Alisema Jombaa na kumpatia Mathew ile simu akaizima.

“Ahsante sana Jombaa. Naomba unisubiri hapa hapa” alisema Mathew na kuelekea ndani lakini ghafla alikutana na Ruby akitoka nje nyuma yake akiwa Gosu Gosu.Mathew alihisi hatari akaichomoa bastola.

“Kuna nini Ruby?

“Mathew nilikuwa nakufuata. Kuna tatizo limetokea.”

“Nini kimetokea? Aliuliza Mathew.

“Mfumo wa SNSA umezimwa. Inaonekana tayari wamegundua tunatumia mfumo wao” alisema Ruby.

“Mathew hawa watu tayari wametungundua na kw amujibu wa Ruby wanaweza wakajua kuwa tuko hapa” alisema Gosu Gosu kwa wasi wasi. Mathew aliwatazama.

Ruby alionekana kuchanganyikiwa.

“Ruby relax. Kwa sasa hebu pumzika. Umefanya kazi kubwa sana kuanzia asubuhi. Jipe mapumziko ya muda mfupi” alisema Mathew na kumtaka Gosu Gosu watoke nje.

“Gosu Gosu kuna kitu kimetokea. Regina kumbe ana simu ambayo anaitumia kwa siri kuwasiliana na watu.”

“Ana simu?

“Ndiyo ana simu. Tayari simu hiyo ninayo”

“Umejuaje kama ana simu? Aliuliza Gosu Gosu.

“Nitakueleza kila kitu lakini kwa sasa ninataka umchukue Regina umpeleke kule katika kiwanda chetu kipya. Mfungie katika chumba na unisubiri hapo. Mimi kuna sehemu ninakwenda nitakuja hapo baada ya muda mfupi” alisema Mathew.

“Sawa Mathew” alisema Gosu Gosu kisha wakaelekea ndani hadi katika mlango wa

chumba cha Regina, Mathew akagonga mlango. Regina alishituka sana alipofungua mlango akakutana na Mathew akiwa na Gosu Gosu.

“Mathew kuna nini?

“Regina kuna dharura imetokea. Kuna mtu ameuawa sehemu Fulani ambaye nataka ukatusaidie kumtambua kisha tutarejea hapa. Utaondoka na Gosu Gosu mimi ninakuja.” Alisema Mathew.

“Ni nani huyo mtu? Aliuliza Regina kwa wasi wasi.

“Tunahisi ni mtu ambaye unamfahamu kwani baada ya kuuawa amekutwa na picha yako. Tunataka utusaidie kumtambua. Ni zoezi la muda mfupi kisha utarudi kupumzika. Samahani kwa usumbufu” alisema Mathew.

“Hakuna tatizo.” Alisema Regina akatoka akaongozana na Gosu Gosu wakaingia garini na kuondoka. Mara tu Gosu Gosu na Regina walipoondoka, Mathew alimfuata Ruby.

“Ruby tafadhali chukua kompyuta yako kuna mahali tunakwenda” alisema Mathew.

“Tunakwenda wapi? Gosu Gosu na Regina wanakwenda wapi? Aliuliza Ruby.

“Ruby please hurry! alisema Mathew.

Ruby alichukua kompyuta zake mbili ambazo huzitumia kila wakati wakatoka. Mathew alimuita Jombaa wakaingia katika gari lingine nao wakaondoka.

“Tunakwenda wapi? Ruby aliuliza

“Subiri kidogo utajua mahali tunakoelekea” alijibu Mathew na safari iliendelea kimya kimya.

****

Gari la jaji mstaafu Perfect Lyimo lilisimama katika taa za kuongozea magari barabarani katika makutano ya barabara za Mjungu na Uhuru. Wakati wakisubiri taa za kuwaruhusu ziwake, dereva wa gari lile

alipigiwa simu akaipokea halafu akampatia Perfect.

“Mzee simu yako”

“Simu yangu? Perfect alishangaa.

“Ndiyo mzee” alijibu dereva na Perfect akaishika ile simu akaiweka sikioni.

“Hallow” alisema.

“Perfect zima simu yako sasa hivi na utoe betri yake”

“Unasemaje Julius? Aliuliza Perfect baada ya kuitambua ile sauti ya upande wa pili.

“Perfect nimekwambia zima simu yako sasa hivi na utoe betri yake” alirudia Julius.

“Sawa” alijibu Perfect na haraka haraka aliizima simu yake akatoka betri halafu akaichukua ile simu ya dereva wake. Bado Julius alikuwa katika laini ya simu.

“Good. Sasa njoo mkutanoni” alisema Julius na kukata simu. Perfect hakuelewa sababu ya kupewa maelekezo yale ya kuzima

simu yake na kutoa kabisa betri.

Safari iliendelea hadi waliposimama tena katika taa za kuongozea magari barabarani za makutano ya barabara ya Upare na Swala. Bado kichwa cha mzee Perfect kiliendelea kuzunguka.

Mara tu taa ya kijani ilipowaka na magari kuanza kwenda ilitokea piki piki ikiwa na watu wawili. Piki piki ile ilionesha kama ninataka kulipita gari la Perfect lakini lilipofika katika usawa wa dirisha la mlango wa

katikati alikokuwa amekaa Perfect, jamaa aliyekuwa amekaa nyuma alitoa bunduki ndogo na kuanza kulimiminia risasi gari la Perfect. Zilimiminwa risasi mfululizo kisha pikipiki ile ikaondoka kwa kasi kubwa. Dereva wa gari la Perfect alipoteza uelekeo na kugonga nguzo ya taa za barabarani. Lilikuwa ni tukio la ghafla sana.

Milio ile ya risasi ilifanya eneo lile liwe tupu kwa muda. Watu waliyaacha magari yao wakakimbia. Baada ya dakika chache za ukimya, watu

walianza kuelekea katika lile gari lililogonga nguzo. Kulikuwa na watu wawili pekee ndani yake. Dereva alitolewa garini akivuja damu, alikuwa amejeruhiwa sana akakimbizwa hospitali. Mtu aliyekuwa amekaa kiti cha nyuma hakuwa na uhai. Alikuwa amechakazwa vibaya kwa risasi kutoka katika bunduki ya wale washambuliaji. Haraka haraka polisi waliokuwa doria walifika eneo lile pamoja na askari wa usalama barabarani. Eneo lilizungushiwa utepe wa njano

kuzuia magari kupita. Baada ya polisi kumpekua yule mtu aliyeuawa ili kumfahamu ni nani walimkuta na vitambulishio kadhaa na wote walishangaa baada ya kugundua mtu yule aliyeuawa ni jaji mstaaafu Perfect Lyimo.

****

Mathew alisimamisha gari nje ya nyumba ya Musa Faraji. Mahali pale ndipo alimleta Faraji Dilele asubuhi.

Alipiga honi mara tatu lakini geti halikufunguliwa. Alishuka garini akatazama kila upande kama kuna mtu. Eneo lilikuwa kimya sana. Alielekea getini akausukuma mlango mdogo wa geti ambao haukuwa umefungwa akaingia ndani. Gari ambalo aliamini ni la Musa lilikuwepo mahali pale pale alipolikuta asubuhi alipomleta Faraji.

Akiwa katika tahadhari kubwa aliusogelea mlango, akabisha hodi lakini kulikuwa kimya. Alibisha mara ya pili lakini hakujibiwa. Kulikuwa na

ukimya mkubwa sana. Alijaribu kukinyonga kitasa cha mlango ukafunguka. Sebuleni kulikuwa na giza.

“Hodi humu ndani” alisema Mathew na mara akahisi harufu ya damu. Aliitoa bastola yake haraka sana. Aliingia mle ndani akapapasa ukutani na kuwasha taa. Alikutana na kitu kilichomshitua sana. Musa na baba yake walikuwa wameuawa kwa kupigwa risasi. Mathew alihisi nywele zikimsisimka. Aliisogelea miili ile akaichunguza, ilionesha

mauaji yale yalifanyika muda mfupi ulipita.

“Mambo yanazidi kuwa magumu.” Aliwaza Mathew kisha akatoka haraka sana mle ndani akarudi katika gari lao akaliwasha na kuondoka kwa kasi kubwa.

“Mathew kuna nini? Aliuliza Ruby baada ya kuioa sura ya Mathew ikiwa na mabadiliko.

Ilimlazimu Mathew kusimamisha gari kandoni mwa barabara. Akavuta pumzi ndefu.

“Mathew” aliita Ruby.

“Nilimlata Faraji Dilele katika nyumba ile.Pale ni nyumbani kwa mtoto wake anaitwa Musa.” Alisema Mathew na kunyamaza.

“Mbona tumeondoka? Hawapo? Aliuliza Ruby. Mathew alimeza mate kulainisha koo.

“They’re all dead” alijibu Mathew.

“Dead?

“Ndiyo. Wote wameuawa, tena inaonesha wameuawa

muda mfupi uliopita kwa sababu bado miili haijapoa”

“Mungu wangu tusaidie” alisema Ruby kwa woga halafu kimya kikatawala.

“Kwani tulikuja kufanya nini kwao? Aliuliza Ruby.

“Nilihitaji msaada kutoka kwa Musa. Ruby kuna jambo ambalo sikuwa nimekueleza. Tumegunudua Regina ana simu ambayo amekuwa anaitumia kuwasiliana na watu mbali mbali”

“Regina ana simu? Ruby alishangaa.

“Ndiyo ana simu”

“Umejuaje kama ana simu?

“Ni mimi niliyegundua. Nilimwambia Mathew, tukatumia mbinu tukaipata simu hiyo.” Alisema Jombaa.

“Haya ni maajabu. Anawasiliana na akina nani?” aliuliza Ruby.

“Kwa mujibu wa Jombaa, Regina alikuwa anawasiliana na mtu akimuonya asiende

msibani kwani anachunguzwa. Baada ya mfumo wa SNSA kuzimwa niliona njia pekee ni kuja kwa Musa ambaye ni mfanyakazi wa SNSA ili atusaidie kuweza kuichunguza simu hiyo kwa kutumia mfumo wa SNSA. Kwa bahati mbaya naye ameuawa.”

“Mathew ulipaswa kuniambia jambo hilo, ningetumia program zangu nyingine tungefahamu kila kitu. Kuzimwa kwa mfumo wa SNSA hakuwezi kutuzuia kufanya kazi zetu. Kila kitu kitaendelea kama kawaida.”

Alisema Ruby. Mathew alimpa Ruby ile simu ya Regina.

“Gosu Gosu amempeleka wapi Regina? Ruby aliuliza.

“Amempeleka sehemu salama kwa ajili ya mahojiano ya kina. Lazima tuwafahamu watu ambao Regina alikuwa anawasiliana nao.” Alisema Mathew

“Mathew nilikuonya tangu awali kuhusu kuwa makini na Regina.”

“Ni kweli. Hata Gavana aliwahi kunipa onyo hilo. Ruby

muda unakimbia hebu ipitie simu hiyo na tujue amewasiliana na akina nani” alisema Mathew.

Haraka haraka Ruby alianza kazi. Mathew aliwasha gari wakaondoka.

“Bastard ! alisema Ruby.

“Kumbe tulikuwa tunafuga shetani.!” Alisema Ruby kwa hamaki.

“Kuna chochote umekipata?

“Alituma jumbe jioni hii.”

“Unasemaje ujumbe huo? Usome kwa sauti” alisema Mathew na Ruby akausoma ujumbe ule.

“Hawa watu bado ving’ang’anizi. Wamefanikuwa kuiunganisha simu ya Perfect na kmpyuta yao. Sasa wanaweza kufuatilia mawasiliano yote ya Pefect”

“Dah ! alisema Mathew.

“Wamewezaje kuunganisha simu ya Perfect na kompyuta yao? Aliuliza mtu aliyetumiwa ujumbe.

“Wanamtumia Ambola. Yule mwanamke ni hatari sana. Anatumiwa pia na hawa jamaa. Muondoeni haraka sana ama sivyo kila kitu kitaharibika” alijibu Regina.

Ilimlazimu Mathew kusimamisha gari pembeni ya barabara.

“Mpigie simu Jackline haraka sana amuondoe Ambola msibani kimya kimya” Alisema Mathew. Ruby alichukua simu akampigia Jackline Mo.

“Ruby” alisema Jackline baada ya kupokea simu.

“Jackline naomba unisikilize vizuri.” Alisema Ruby.

“Ninakusikiliza Ruby”

“Naomba haraka sana tena kimya kimya umuondoe Ambola hapo msibani.”

“Kuna nini Ruby?

“Ambola yuko katika hatari kubwa. Ukichelewa kuna watu watamuua” alisema Ruby.

“Mungu wangu. Kuna watu wamekuja kumchukua hapa sekunde chache zilizopita wanasema wametumwa kuzungumza naye kuhusu masuala ya mazishi ” alisema Jackline.

“Jack fanya haraka sana muokoe Ambola, watu hao lazima ni wale waliotumwa kuja kummaliza” alisema Ruby na kukata simu.

“Tayari kuna watu wamefika msibani na kumchukua Ambola wanadai

wanataka kuzungumza naye.” Alisema Ruby.

“Imekuwa vyema Jackline yuko karibu. Ataumaliza mchezo huo” alisema Mathew .

“Do you trust her? Aliuliza Ruby.

“Yes I do.”alijibu Mathew.

“Ruby hilo suala la Ambola limekwisha tujielekeze katika hii simu ya Regina” alisema Mathew.

“Mathew mimi bado nina wasi wasi sana na yule Jackline. Sina hakika na

maisha ya Ambola. Kwa nini tusiende mara moja tukahakikisha Ambola yuko salama? Aliuliza Ruby.

“Ruby please trust me. Simfahamu vyema Jackline lakini baada ya kumuona kwa mara ya kwanza nina uhakika mkubwa Ambola yuko salama. Tafadhali jielekeze katika simu ya Regina. Tafuta watu aliowasiliana nao” alisema Mathew.

“Hakuna namba yoyote iliyohifadhiwa katika laini ya simu.Ila inaonesha Regina

amekuwa akiwasiliana na namba moja tu” alisema Ruby na kuendelea kubonyeza kompyuta yake.

“Lucy Mzumile” alisema Ruby.

“Mke wa Gavana. Ruby una hakika?

“Ndiyo. Namba hii ya simu ambayo Regina alikuwa anawasiliana nayo imesajiliwa kwa jina la Lucy Mzumile.”

“Jesus ! alisema Mathew na kuinamisha kichwa chake.

Aliwasha gari wakaendelea na safari.

“Ninataka nikamchukue Gosu Gosu niende naye kumtafuta Lucy.Jombaa nitakuacha hapo uendelee kumlinda Regina” alisema Mathew.

****

Taratibu gari alilokuwa anaendesha Gosu Gosu lilipunguza mwendo baada ya kulikaribia geti kubwa jeusi. Ndani ya ukuta mrefu kulionekana majengo kadhaa ambayo ujenzi wake ulimalizika tayari. Hiki kilikuwa ni kiwanda kipya cha kutengeneza maziwa ambacho kilikuwa kinasubiri kufungwa mashine ili uzalishaji uanze. Kiwanda hiki ni moja ya uwekezaji unaofanywa na Mathew Mulumbi ukisimamiwa na Gosu Gosu

kama msimamizi mkuu wa Mulumbi Group of companies.

Gosu Gosu alishusha kioo akazungumza na mlinzi. Walionekana kufahamiana kwani walitaniana kidogo halafu mlinzi yule akafungua geti gari likaingia ndani.

“Hapa ni wapi? Aliuliza Regina.

“Tushuke. Safari yetu imeishia hapa” alisema Gosu Gosu. Regina alianza kuingiwa na wasi wasi. Eneo lile lilikuwa kimya sana, hakukuwa na

dalili zozote za kutokea mauaji.

“Mauaji yamefanyika wapi? Aliuliza Regina.

“Follow me” alisema Gosu Gosu.

Regina alimfuata Gosu Gosu kuingia katika jengo la utawala ambako kulikuwa na ofisi mbali mbali. Tayari kila ofisi iliwekwa samani za kupendeza.

“Hiki ni kiwanda cha nini? Regina aliuliza baada ya kuzipita ofisi kadhaa.

Gosu Gosu alifungua mlango wa moja ya ofisi akamtaka Regina aingie ndani akaketi kitini.

“Yuko wapi mtu aliyeuawa? Aliuliza Regina.

“Mauaji hayajatokea hapa. Tunawasubiri akina Mathew wamekwenda kuuchukua mwili watakuja nao hapa hapa” alisema Gosu Gosu.

“Kwa nini tusingeenda huko mahali yalikotokea mauaji ili kuokoa muda?

“Ni hatari sana kwako kuonekana huko” alijibu Gosu Gosu.

Ulipita ukimya mfupi, Regina akauliza.

“Una watoto wangapi Gosu Gosu?

“Sina mtoto hata mmoja. Wewe una wangapi?

“Mimi pia sina hata mmoja. Unasubiri nini?

“Bado sijapata mwanamke wa kuzaa naye mtoto.”

“Pole kwa kilichokutokea kwa mpenzi wako.”

“Usijali yamekwisha pita hivi sasa ninajielekeza katika masuala mengine ya muhimu” alisema Gosu Gosu.

Regina aliinuka kutoka pale sofani akamfuata Gosu Gosu.

“Gosu Gosu nahitaji kwenda maliwato. Nielekeze tafadhali” alisema Regina.

“Twende nikakuoneshe”

“Nielekeze tu nitakwenda mwenyewe. Sitaki nikusumbue” alisema Regina. Tayari Gosu Gosu alikwisha

anza kupiga hatua kutoka nje Regina akamfuata. Alimuelekeza msalani halafu akasimama nje akimsubiri. Baada ya dakika kadhaa Regina alifungua mlango akatoka.

“Ouh kumbe ulikuwa unanisubiri?

“Ndiyo. Tunakulinda hata ukiwa chooni kuhakikisha unakuwa salama” alisema Gosu Gosu kisha wakaanza kurejea katika ile ofisi. Mara Regina alisimama akaishusha chini suruali aliyoivaa.

“Ninawashwa mapajani.”alisema Regina huku akijikuna mapajani. Gosu Gosu mapigo ya moyo yalianzaa kwenda kasi baada ya kuyashuhudia mapaja yale meupe. Regina alipandisha juu zaidi fulana yake na kumfanya Gosu Gosu aione nguo yake ya ndani ya rangi nyekundu. Regina alingiza mkono mmoja ndani ya nguo yake ya ndani akajikuna. Gosu Gosu alisisimkwa mwili.

“Regina twende ndani ukatoe nguo. Yawezekana umekutana na wale wadudu

wanaowasha” alisema Gosu Gosu. Regina aliipandisha juu suruali ile akatembea kwa haraka hadi katika ile ofisi. Mara tu alipoingia alivua fulana akaitupa chini. Gosu Gosu alikishuhudia kifua kilichobeba matiti yaliyojaa. Regina hakuishia hapo aliivua suruali akabakiwa na nguo ya ndani.

“Gosu Gosu naomba unikune kwa hapa mgongoni” alisema Regina. Gosu Gosu alimsogelea akaanza kumkuna mahali alipoelekezwa. Mara Regina aliinama na kumgoga

Gosu Gosu kwa makalio yake halafu akaguna.

“Gosu Gosu mbona ikulu kumekasirika namna hiyo? Aliuliza Regina lakini Gosu Gosu hakumjibu kitu. Ambola aligeuka akaupeleka mkono wake ikulu kwa Gosu Gosu.

“Gosh ! it’s so hard. Samahani Gosu Gosu”

“Usijali” alijibu Gosu Gosu.

“Unadhani itawachukua muda gani akina Mathew kufika hapa?

“Sina uhakika yawezekana ikawa zaidi ya dakika kumi”

“Tunaweza kufanya hata mzunguko mmoja kabla hawajafika.” Alisema Regina huku akifungua mkanda wa suruali ya Gosu Gosu ambaye haraka haraka aliivua suruali yake akaitupa chini. Mtanange usio na maandalizi ulianza. Regina aliikamata meza na kumpa nafasi Gosu Gosu ya kutawala mchezo kutokea nyuma. Ulikuwa mtanange mzito. Gosu Gosu alikaribia kufunga goli akamjulisha Ambola na mara alisukumwa

akaanguka chini. Regina aliinyakua bastola iliyokuwa mezani. Gosu Gosu alipatwa na mshituko uliomfanya ikulu kupoe ghafla.

“Regina” alisema Gosu Gosu baada ya kumuona Regina amemuelekezea bastola.

“Shut up ! alifoka Regina. Gosu Gosu hakuamini kile kilichotokea. Alihisi kama yuko ndotoni. Sura ya Regina ilibadilika. Hakuwa Regina yule ambaye muda mfupi uliopita alikuwa katika

mtanange mzito na Gosu Gosu.

“Regina please ! aliomba Gosu Gosu.

“Shut up ! Wafu hawazungumzi ! alisema Regina.

“Regina weka silaha chini tafadhali. ! Alisema Gosu Gosu huku akitaka kunyanyuka.

“Piga magoti Gosu Gosu. Usitake nikuue kabla ya wakati. ! Alifoka Regina. Gosu Gosu alipiga magoti. Bastola iliyofungwa kiwambo cha sauti

ilielekezwa kwake. Kidole cha Regina kilikuwa katika Kizinga tayari kabisa kuachia risasi na itakayochukua uhai wa Gosu Gosu.

“Drop your gun !

Sauti kali ikitokea mlangoni ilimuamuru Regina.

“Drop your gun! ilisema sauti kali ya Mathew Mulumbi aliyesimama mlangoni akiwa na bastola mkononi.

“Taratibu weka chini silaha yako ! aliamuru Mathew.

Regina alianza kubonyea chini kwa ajili ya kuweka silaha kama alivyoamriwa, lakini kabla mkono haujafika chini aligeuka ili amkabili Mathew. Gosu Gosu aliruka mithili ya Kima akamtandika teke zito Regina akaanguka chini. Kabla Regina hajageuka Gosu Gosu tayari alikwisha mkalia juu akaisukuma bastola pembeni na kuanza kumporomoshea Regina kipigo kizito sana hadi Mathew alipomshika na kumuondoa. Sakafuni kulisambaa nywele ambazo Gosu Gosu aling'oa

kichwani kwa Regina wakati akimshushia kipigo.

“Imetosha Gosu Gosu. Vaa nguo zako tafadhali” alisema Mathew. Gosu Gosu alikuwa na hasira kama Nyati aliyejeruhiwa. Alivaa nguo zake haraka haraka.

“Ruby mvalishe Regina nguo zake” alielekeza Mathew. Ruby alimvisha Regina nguo zake. Alikuwa anavuja damu.

“Gosu Gosu chukua waya mfunge Regina katika kiti” alisema Mathew. Gosu Gosu alimvuta Regina akamketisha

kitini alimtazama kwa hasira halafu alichukua waya uliokuwemo mle ndani akamfunga Regina.

Mathew alimkabidhi Jombaa bastola.

“Jombaa ninakukabidhi kazi. Huyu mwanamke anapaswa kulindwa asitoke humu ndani. Mimi na Gosu Gosu tutarejea muda si mrefu. Ruby atabaki pia hapa. Tafadhali kuwa makini sana na huyu mwanamke” alisema Mathew.

“Mathew usihofu kabisa. Hakuna tatizo litakalotokea” alisema Jombaa.

“Ruby usiwe na wasi wasi, Jombaa atakulinda utakuwa salama. Sisi tunakwenda kumtafuta mke wa Gavana” alisema Mathew kisha wakatoka wakikimbia kuelekea katika gari lao wakaondoka.

“Mathew I’m sorry. Sijui ni shetani gani alinipitia.”alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosi sijafurahishwa na kile nilichokishuhudia mle chumbani. Tutazungumza

baadaye, kwa sasa tujielekeze katika kile kilichopo mbele yetu. Tumegundua Regina ana mawasiliano na mke wa Gavana. Tunakwenda kumchukua mwanamke hyo tumuhoji. Jambo lingine, Ambola tayari amekwisha fahamika kuwa anashirikiana nasi. Nimempa maelekezo Jackline ahakikishe Ambola anakuwa salama" alisema Mathew.

"Mathew ninahisi aibu kwa jambo la aibu nililolifanya. Sikujua kama mwanamke yule ni hatari kiasi

hiki. Tulimpa hifadhi nyoka ambaye anataka kutugonga wenyewe. Ninajilaumu sana kwa ujinga nilioufanya. Kama si wewe kutokea hivi sasa ningekuwa nimekufa" alisema Gosu Gosu.

"Gosu Gosu si mara ya kwanza leo ninakuonya kuhusu udhaifu kwa wanawake. Sifahamu nini kilichotokea mle ndani lakini ni wazi kuna jambo lilifanyika ambalo si zuri hasa kwa wakati huu ambao tuko katika mapambano" alisema Mathew.

“Mathew I’m so stupid ! Natamani nijitukane matusi yote ya dunia hii. Nilifanya jambo la kijinga sana” alisema Gosu Gosu na kumueleza Mathew kile kilichotokea.

“Nimekuelewa Gosu Gosu na kama ndugu yako sintaacha kukukumbusha kuhusu kuwa makini na wanawake. Jitahidi kudhibiti tamaa zako za mwili. Kwa sasa litoe tukio lile akilini mwako na tujielekeze katika mapambano. Mlima tunaopanda unazidi kuwa mzito sana. Hata hivyo tunavyozidi kukutana na

magumu mengi ndivyo tunavyozidi kuukaribia ushindi. Tuendelee kupambana. Mungu yuko nasi.” Alisema Mathew.

****

Tayari watu wote waliotakiwa kuhudhuria kikao cha dharura saa moja jioni, walikwisha wasili Ngome. Kila mjumbe alichukua nafasi yake katika chumba cha mikutano.Ni viti viwili tu ambavyo havikuwa na watu.Watu wengine wanne,

walionekana katika runinga nne zilizokuwa upande wa mbele wa chumba kile wakifuatilia kikao kile kwa njia ya mtandao. Muziki wa ala ulisikika kwa mbali huku kukiwa na mazungumzo ya chini chini miongoni mwa wajumbe. Mwenyekiti wa kikao hakuwemo ndani ya chumba cha mikutano.Alikuwa ofisini kwake akisubiri kujulishwa kuwa mjumbe mmoja waliyekuwa wanamsubiri tayari amefika.NIU Perfect Lyimo aliyekuwa anasubiriwa.

Ilipofika saa moja na dakika ishirini bila Perfect kutokea. Mwenyekiti alitoka ofisini kwake akaingia katika chumba cha mikutano walimokuwemo wenzake.

“Ndugu zangu habari za jioni” alisema Mwenyekiti baada ya kuketi katika kiti chake.

“Tumekutana tena hapa kama tulivyokubaliana katika kikao cha alfajiri ya leo. Kwa bahati mbaya wajumbe wote wa kikao hiki wamefika isipokuwa Perfect ambaye

nimeambiwa yuko njiani anakuja. Kwa kuwa kanuni yetu inatutaka tuzingatie muda, tunaendelea na kikao." Alisema Mwenyekiti halafu akawatazxama wajumbe.

"Katika kikao cha asubuhi, tulipewa taarifa ya kile kilichotokea usiku wa kuamkia leo katika moja ya nyuiumba zetu, *safe house 6*. Nilimpa majukumu mkuu wetu wa idara ya ulinzi na usalama aandae taarifa ya kina kuhusiana na tukio lile vile vile mikakati na hatua mbali mbali ambazo amezichukua yeye na

idara yake. Karibu Julius kwa taarifa ya kina.” Alisema Charles Ombe mwenyekiti wa kikao kile.

“Nitaanzia pale nilipoishia asubuhi. Niliwaeleza kuwa kupitia *Asset 12* tulifanikiwa kugundua kwamba Gavana alikutana usiku wa kuamkia leo na watu wawili. Mathew Mulumbi na Faraji Dilele. Nilianza kuchukua hatua asubuhi ile ile kwa kumteka Gavana na kumpeleka katika moja ya nyumba zetu kwa mahojiano. Haikuwa rahisi kumfungua

Gavana lakini vijana wetu wamefanya kazi kubwa na hadi jioni ndipo alipokubali kufunguka kueleza ukweli kuhusu Mathew Mulumbi. Nimezungumza na vijana wangu muda mfupi uliopita bado wako mahali na na Gavana wanamsubiri Mathew Mulumbi. ” Alinyamaza Julius baada ya mmoja wa wajumbe kunyoosha mkono akitaka kuliza swali.

“Una hakika Mathew Mulumbi atatokea?

“Ndiyo. Uhakika ni mkubwa kwani kwa mujibu wa vijana wangu, Gavana amesema ana miadi ya kukutana na Mathew Mulumbi sehemu Fulani usiku wa leo hivyo umewekwa mtego mahali hapo. Mara tu Mathew atakapotokea basi atakamatwa. Tukimpata Mathew Mulumbi hatutakuwa na hofu tena” alijibu Julius halafu akanyamaza kwa sekunde kadhaa. Alikuwa anapokea taarifa Fulani kupitia kifaa chake cha kupokelea simu alichokiweka

sikioni. Baada ya muda akasema.

“Samahani ndugu zangu nimepokea taarifa ambayo si nzuri. Kuna jambo limetokea muda mfupi uliopita. Tulimtegemea mwenzetu jaji Perfect afike hapa lakini hataweza kufika hapa tena kuungana nasi katika kikao.” Alinyamaza kidogo halafu akasema.

“Perfect is dead”

Taharuki kubwa ilitokea ndani ya kile chumba. Kila mtu alishangaa.

“Julius hebu tueleze kwa kina nini hasa kilichotokea? Perfect ameuliwa na nani? Aliuliza mjumbe moja ambaye alikuwa anafuatilia kikao kile kwa mtandao.

Julius Mukoke aliinamisha kichwa kwa sekunde kadhaa halafu akasema.

“I did. I killed him.”

Wajumbe wote walihisi baridi ya ghafla. Mara Charles Ombe aliinuka na kumtazama Julius kwa hasira.

“Who are you? Nani amekupa mamlaka ya kutoa hukumu ya kifo? Aliuliza Charles kwa sauti kali. Sura za wajumbe wote zilionesha mshangao mkubwa.

“Relax everyone” alisema Julius.

“Nakuuliza wewe ni nani hata ukaanza kutoa hukumu ya kifo ndani ya mtandao huu? Aliuliza tena Charles Ombe.

“Naomba mnisikilize ndugu zangu. Naomba mnipe dakika chache mnisikilize” aliomba Julius. Bado

minong’ono iliendelea hadi pale mmoja wa wajumbe aliyekuwa anafuatilia kwa mtandao alipoomba Julius apewe nafasi ya kueleza sababu za kumuua Perfect.

“Usiku huu, kupitia vyanzo vyangu nimepokea taarifa isiyo na shaka hata kidogo kuwa Bernadetha aliuawa na Joseph Tshibanga” alisema Julius na kuwaacha watu wote midomo wazi.

“Joseph? That’s impossible! Alisema Charles Ombe.

“Baada ya kumuua Bernadetha, Joseph Tshibanga naye aliuliwa na mtu anaitwa Thomas Ngalula. Nimeambiwa huyu ni mfanyakazi katika ubalozi wa Congo hapa Tanzania na ni mmoja wa watu walio katika mtandao wa Congo mpya. Simfahamu huyo Thomas ila tunaendelea kuchunguza na hadi kufika kesho atakuwa amepatikana.” Julius alinyamaza kidogo. Bado nyuso za wajumbe zilikuwa na mshangao. Julius aliendelea.

“Huyo Thomas Ngalula kwa sasa anashirikiana na akina Mathew. Baada ya mauaji hayo kufanyika, Gosu Gosu alirejea kwa akina Mathew Mulumbi ambao wamepiga kambi yao hapa Dar es salaam mahali pa siri. Taarifa niliyoipata inasema kuwa usiku huu simu ya Perfect imeunganishwa kitaalamu na kompyuta ya akina Mathew hivyo kuwawezesha kufuatilia mawasiliano yake yote ya simu.”

“What? Alisikika mmoja wa wajumbe.

“Hawa jamaa wanatumia teknolojia kubwa kwani kwa msaada wa Faraji Dilele wameweza kuingia katika mfumo wa SNSA bila sisi kufahamu na wanautumia mfumo huo kufanikisha mambo yao mbali mbali. Baada ya kupata taarifa hiyo nilifanya maamuzi ya kwanza kwa kumtaka Perfect azime simu yake na kutoa betri ili kuwazuia akina Mathew kuendelea kufuatilia mawasiliano yake. Pili

nilituma vijana wangu kwenda kumuua kabisa kwa sababu tayari ni mtu hatari kwetu. Tatu nilituma vijana wangu kumfuata Faraji Dilele ambaye alikuwa amejificha nyumbani kwa mwanaye Musa Faraji mfanyakazi wa SNSA. Taarifa niliyoipata ni kuwa Faraji na mwanaye wote wameuawa. Kwa sasa tayari kuna timu iko kazini kutafuta maficho ya akina Mathew Mulumbi.”alisema Julius.

“Dah ! sikujua kama mambo yako namna hii. Hawa watu kumbe wamepiga hatua

kubwa namna hii. Hata hivyo bado sioni sababu ya kumuua Perfect. Kama simu yake tayari ilizimwa angetafuta simu nyingine. Hakuna sababu ya msingi iliyopeleka Perfect akauawa" alisema mmoja wa wajumbe.

"Kuna kitu kimoja ambacho hamkifahamu. Perfect alikuwa mtu hatari sana kwetu. Kuna yule msichana Ambola kutoka mtandao wa Congo ambaye alikuwa akiishi nyumbani kwa Perfect, yule anatumiwa na akina Mathew. Perfect alikuwa

na mahusiano ya kimapenzi na yule msichana bila kufahamu kuwa anatumiwa na maadui zetu. Kama tungemuacha hai Perfect basi tungekuwa katika hatari kubwa sana. Misheni nzima ingeharibika. Mnataka hilo litokee? Alihoji Julius. Chumba kilikuwa kimya. Baada ya muda mwenyekiti akasema.

“Maelezo hayo ya mwisho yametoa picha pana kabisa ya hatari iliyokuwepo mbele yetu na sasa ninakuunga mkono kwa hatua uliyoichukua. Tumeumia sana kwa kifo cha

mwenzetu lakini ulichokifanya ndicho kilichotakiwa kufanywa. Misheni hii lazima tuilinde kwa gharama zozote na kuhakikisha tunaifikisha mwisho. Pamoja na kukupongeza nataka kufahamu wapi alipo Ambola kwa sasa? Una mpango gani na Gavana?

"Tayari nimetuma timu kwenda kumchukua Ambola. Yule naye atatusaidia sana kufahamu mahali alipo Mathew Mulumbi. Kuhusu Gavana, usiku wa leo atauawa kwa sababu hatutamuhitaji

tena. Nina uhakika mkubwa usiku huu wa leo Mathew Mulumbi na kundi lake watapatikana. Hawajui kama tayari tumewazuguka na muda wowote kuanzia sasa tutafahamu mahali walipojificha” alisema Julius kikao kikaendelea.

NDUGU MSOMAJI USIKOSE SEHEMU IJAYO. .